Swahili
65-1204

Unyakuo
The Rapture

December 4, 1965
Yuma, Arizona USA

Na
William Marrion Branham

www.biblebelievers.org/messagehub

Kitabu hiki kinaweza kutengenezwa upya na kusambazwa, lakini hakiuzwi, kama kilivyowekewa leseni chini ya Creative Commons (by-nc-nd) kwenye www.CreativeCommons.org.

Unyakuo

[1] Mkutano huu hapa-hapa Yuma. Ni heshima kubwa kupata mwaliko huu wa kurejea tena! Mara ya mwisho tulipokuwa hapa, tulikuwa na wakati wa burudiko sana, na ndipo nika … nilipofahamu kuwa ilinipasa kurejea tena huku, ilinifanya nijisikie vizuri ajabu. Kusikia shuhuda na haya maneno mazuri kutoka kwa watu, ni kama inakuinua kidogo A …

[2] Billy aliniambia kuwa yule ndugu kutoka Las Vegas aliyetaka tukutane pale kwenye mkutano, nimwone mara tu baada ya kumalizika kwa ibada hapa. Yeye anasema, tunao muda fulani, ambao tunaweza kujipenyeza wakati wa mwezi wa Januari kabla ya mkutano wa Phoenix (Unaona?) kuja-kuja Las Vegas. Na hivyo mara zote tumetaka kufika pale.

Naamini Ndugu Art Wilson alikuwa anakaa kule siku nyingi zilizopita, au huenda akawa bado anakaa kule. Na yeye-yeye aliniomba nipande kwenda kule, yeye na Dada Wilson. Na sikuipata hiyo nafasi, hivyo huenda hii ikawa ndiyo nafasi ambayo ningeweza kuja.

[3] Unaweza kuona tu Billy Paul an Ndugu Roy Borders (Nadhani yupo mahali fulani hapa. Mtu mmoja alisema Ndugu Roy alikuwepo.) Ndugu Pearry, Lee, au yeyote kati yao, wataweza kukuambia, na kupanga tu tarehe za sisi kuja.

[4] Sasa, nimewaona hapa wahudumu kitambo kidogo kilichopita, ambapo nimefurahia sana kuonana na ndugu zangu. Laiti ningelikuwa na wakati … tuende nyumbani pamoja nanyi, kwani mnajua pale kuna mpishi aliye bora kupita wote nchini. Hilo ni jema. Na nina …

[5] Na sasa kuna mambo mawili, dhidi ya Ndugu Pearry kweli usiku huu. Hizi ni alama mbili dhidi yake sasa mojawapo ya kuingilia kile kipaza sauti nje pale wakati … Una … Unahesabiwa hatia juu ya hilo Ndugu Pearry. Sidhani kuwa u mwenye hatia kikwelikweli, lakini una … “Mtu fulani alikuwa anajiandaa kuzungumza.” Hilo lilikuwa zuri.

[6] Na hivyo, ndipo tena, alikwenda nje pale alikuwa anazungumza; akasema, “Sema.” Anamweleza Ndugu Collins au baadhi yao, kasema, “Kile chakula cha jioni kilikuwa kizuri,” lakini kasema, “Ninakwambia” kasema, “yule mtu sharti awe Mhispania au kitu kama hicho, au Mmeksiko. Hiyo ilikuwa ni pilipili kali kuliko yoyote niliyowahi kuonja,” akaendelea kusema hivyo, na alikuwa anaongea na mpishi mkuu wa hoteli. Huyu akasema, “Mimi ndiye mpishi mkuu”.

[7] Kwako hiyo ni Texas. Tutamweka sawa akiwa hapa Arizona baada ya muda si mrefu, au sivyo, kama atakuwa pamoja nasi-akiwepo hapa.

[8] Ni vema hasa kuwa hapa. Nadhani hayo hayasikiki kama mizaha, ila ni ucheshi. Ambapo Bwana Mwenyewe alikuwa na hali ya ucheshi, unajua. Yeye alisema, “Herode … Nenda kamwambie yule mbweha (Unaona?) Leo natoa-natoa mapepo, kesho Ninafanywa mkamilifu”. Hivyo kama alikuwa-alikuwa na ucheshi, mbona, haitatutia uchungu. Sidhani, mara chache.

[9] Na sasa, tume-tumechelewa kidogo. Kwa kawaida huwa nina-ninahubiri kadiri ya kama masaa manne. Hivyo kwa kujua tu heshima ya ndugu na dada hapa wa mkutano huu, tutakatisha kufupisha muda huo usiku huu.

Na ndipo … nilimwambia Terry; nikasema … Yeye alisema, “Nini … Tumeweka nini kwenye kanda ya masaa mawili?”

[10] Nikasema, “Hapana, Terry, hii ni-ni karamu”. Nikasema, “Kama dakika thelathini au arobaini, wahubirie watu pale-juu ya kitu fulani.” Hilo, hata hivyo ninajaribu, kila mara, hali nikijua hivyo.

[11] Wakati nilipokuwa mvulana mdogo, watu walikuwa wanakuja kusikiliza kwa sababu kwamba nilikuwa ni mhubiri mvulana, kijana tu, kijana mdogo. Na wangesema, “Vema, Billy Branham … Unajua, kijana tu, hakuwahi kujua-hakupitia kamwe shule na hana elimu. Na wangejitokeza kusikia maneno yangu ya kuvunjavunja, Kiingereza changu cha Kentucky. Na-na hivyo wali-“hits zangu na “hits” na “totes” na carry”

Kama katika mojawapo ya mikutano hapa kitambo kifupi kilichopita walisema, “Sote tutasimama na kuimba Wimbo wa Taifa”.

[12] Niliamka na kusema, “Kwa ajili ya nyumbani kwangu kwa kizamani mbali kutoka hapa. Hilo ndilo taifa pekee nijualo habari zake, hivyo ilikuwa ni Wimbo wa Taifa kwa kadiri ninavyohusika.

[13] Hivyo sasa, ingawa baada ya kukua, zaidi kiumri, mbona, vema, tuna, unafahamika, inabidi uwe kitu zaidi ya hicho. Mnaona, tukimchukua … Paulo alisema hilo, “Nilipokuwa mtoto, nilisema kama mtoto na nikawaza kama mtoto.” Unatenda kama mtoto. Lakini unapozidi kukua, ndipo unapoanza hatua zako kadha za kwanza za kutembea na ukipepesuka na kuanguka, na kuinuka na kujaribu kutembea tena. Na ndipo una-baada ya kitambo kidogo unafikia kiasi cha kutembea kwenye msitari ulionyooka. Na hilo ndilo litupasalo kufanya kama askari wa msalaba. Sasa wakati umefika wa kutembea katika msitari ulionyooka moja kwa moja katika ile njia kuu hadi Utukufuni.

[14] Ninaamini kuwa tunaishi katika matukio ya kumalizia historia ya ulimwengu. Naamini kwa kweli kuwa kuja kwa Bwana kumekaribia zaidi labda kuliko tunavyodhani. Hivyo sasa, kwa muda wako kama dakika thelathini hivi au kitu kama hicho, ningependa kuvuta usikivu wenu kwenye

tu, kitu fulani cha kutengenezwa, mfumo fulani wa kidhehebu, ungamo fulani mfumo fulani wa imani ya kanisa ambayo imeongezea. Wanaelewa, Baba, kuwa inahitaji Neno la Mungu ambalo ni safi, lisiloghoshiwa. Kila kitu kingine kitapita, hata mbingu na nchi, lakini Neno haliwezi. Na kama tukiwa hilo Neno, dunia itapita kutoka chini yetu lakini sisi hatutapita kamwe kwa sababu tu lile Neno, Bibi Arusi wa Bwana Arusi.

[213] Namwombea kila mmoja, kwamba utamridhia kila mmoja wao, Baba, hayo ni maombi yangu ya dhati. Na samahani Baba kwa kuwa nilikuwa na fadhaiko usiku huu, nilipofika kwa kuchelewa, nikiwa nimeshtuka, nikawa nikisema maneno yaliyovunjika na kukatika. Kwa njia moja au nyingine Roho Mtakatifu Mkuu, yaunganishe pamoja katika njia Yako Mwenyewe ya Kiungu, na upeleke katika mioyo ya watu, kutoka moyoni mwangu, na madhumuni na sababu iliyo katika moyo wangu, nilio nayo juu yako. Je utafanya hivyo Bwana ? Na waokoe wale wawezao kuokoka wavute kwako, Bwana. Na twaomba tuwe tayari kwa ajili ya saa ile ya Unyakuo ambayo punde si punde itawadia. Kwani ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu awabariki.

Sasa, kwa mwenyekiti wa mkutano.

Kama umekuwa mkweli kwa Mungu,

Nyumba yako katika Utukufu itakuwa njema na ing'aayo.

Nafsi yako iliyonyakuliwa itaiona!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika,

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika,

Jenga matumaini yako katika mambo ya Milele.

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Nataka uinamishe kicha chako kwa muda mfupi tu sasa.

Usitamani mali za dunia hii zisizofaa,

Ambazo zinaoza haraka,

Tafuta kupata hazina ya Mbinguni,

Hivyo havipiti kamwe!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Jenga matumaini yako katika mambo ya Milele

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

[211] Hali mmeinamisha vichwa vyenu na mkiwa na hili mawazoni hali tukijua kuwa tumeinamisha vichwa vyetu kuelekea mavumbi ambayo tulitolewa kutoka ndani yake, siku moja tutarejea, ukijua kuwa unayo nafsi ndani pale ambayo itajibu kwa Mungu. Na kama ukijisikia kuwa hujawa tu tayari kwa Unyakuo huo, kama ungekuja usiku huu, na ungetaka ukumbukwe katika maombi, inua tu mkono wako. Nafasi haitoshi hapa tikiita watu waje madhabahuni. Madhabahu yako imo moyoni mwako, hata hivyo. Inua mkono wako, Mungu akubariki, wewe, wewe. Jamani.

Unajisikia sijawa tayari, Ndugu Branham, Nina-nina, kweli, Nina-nina-ninataka kuwa Mkristo. Nimejaribu kuwa . lakini daima kumekuweko na kitu kilichopungua. Nina-Ninajua kuwa si-sipo mahali pale iliponipasa kuwa".

Unirehemu Mungu, Nainua mkono wangu. Unirehemu. Sasa, mikono kama ishirini hivi imeinuliwa tayari, katika kikundi hiki kidogo. Mingine zaidi inainuliwa.

[212] Mpendwa Mungu, Wewe unajua kile kilicho nyuma ya ule mkono, chini pale, chini ya moyo, naomba mpendwa Mungu. Kuna jambo moja tu ninalowajibika nalo, hilo ni kueleza ile Kweli.. Na, mpendwa Mungu, wanapenda kuokolewa. Wao hawataki kitu hiki ambacho ni msisimko fulani

Andiko ambalo ningetaka kulitumia kwa-somo na-na kutumia mengine hapa. Nili …

Nilipokuwa nimeketi pale nyumbani siku fulani, nilikuwa ninafikiria juu ya wazo hili. Ndipo nikawaza, "Vyema, sijui, kuhubiri kutoka kwenye Andiko hili lote, nitachukua tu sehemu yake na kwa ajili ya hizi ibada fupi fupi kama tuliyo nayo usiku huu. Nataka niseme jambo moja wakati mnapofungua Zaburi ya-ya kwanza-Zaburi 27, nataka kusoma, aya tano za kwanza.

[15] Ningetaka kusema hivi kuhusiana na mikutano hii ya Wafanyabiashara-Wafanyabiashara wa Injili Nzima.

Ndugu yangu Pearry alikuwa anazungumza juu ya vitabu na kadhalika, na vitabu vipya walivyo navyo. Ni wangapi wanaokumbuka wakati tulipokuwa na kanda na nilihubiri hapa Phoenix, kwenye mojawapo ya mikutano, kuhusu "Mabwana Huu ni Wakati Gani?" Sasa huo ndio uliokuwa mwanzo wa kile kitabu (Mnaona?) wakati lili-hili lilipotukia.

[16] Kuna madhihirisho ya Kiungu mengi kupindukia ya Neno la Mungu lililoandikwa la saa hii kiasi kwamba haiwezekani kusiweko jambo linalokaribia kutukia kwetu sasa. Tupo tu-ni halisi kupindukia. Mnaona, yale mambo ambayo una … Ingekuwa jambo la kukushtusha kukufahamisha hayo, yale halisi yanayotukia. Wengi wenu mlio wageni huenda mnawasikia hawa watu wakiamka na kutoa-wanatoa maoni yao kuhusu Ujumbe wa saa hii na kadhalika. Kitu wanachokifikia, ni ahadi ya Mungu ya saa hii, kuwa aliahidi kile ambacho angekifanya, na tunamwona Yeye Kimaandiko akithibitisha kikamilifu tu kile ambacho alisema angekitenda kwa jinsi ile ile. Ilitabiriwa, inagonga pale pale tu, kikamilifu kila mara, kwa sababu ni Mungu anayesema hilo.

[17] Kama mtu fulani, sijali yeye alikuwa nani, angejaribu kutoa utabiri wa namna hiyo, … Ni mara moja kati ya milioni kumi ambapo mtu angekuambia kuwa jambo fulani lingetukia na litukie; inge-ingetukia wakati fulani, ni mara moja kati ya milioni kumi. Na kisha pale mahali ambapo lingetukia ingekuwa kama mara moja kati ya milioni mia moja.

Na ndipo, muda ambao lingetukia, na kuendelea. Na jinsi ambavyo lingetukia na nini kingetukia na kadhalika, hiyo ni mbali sana na kule kubahatisha. Wakati tunapoona likiwa hivyo kikamilifu kila wakati, basi ni Mungu.

Na ndipo tunageuka nyuma kuja kwenye Maandiko. Linaweza likaonekana geni kwetu, lakini tunageuka nyuma kwenye Maandiko bila hata kujua tuangalie wapi, na Roho Mtakatifu analileta kwenye uwazi na huwa tu

analiweka Neno lote pamoja, anaweka sura pale ya kutuonyesha tu ile saa tunayoishi. Tuko kwenye mabadiliko ya majira.

[18] Tuko-tuko penye kona. Ni rahisi wakati mtu anapokata kona-ya fundi mwashi-anakata kona na kuanza … Kila mtu anayapanga matofali moja kwa moja chini katika safu hiyo hiyo, kama dhehebu fulani linaanza kubingirika chini kwenye safu, ni sawa; lakini unapowafikia linageuka pale unapopasa kugeukia nyuma upande mwingine …

Sasa, Mungu hajengi ukuta; Yeye anajenga nyumba. Unaona? Na kuna njia za mikato nyingi na kona nyingi ambazo Yeye amezitabiri hapa katika Biblia. Na ni hizo kona … Mtu yeyote angeweza kujaribu kupiga kona, lakini yabidi iwe kama ilivyo kwenye ramani ya jengo. Kama haiko hivyo, yabidi ichanwechanwe tena.

[19] Basi tu-tunamtukuza Mungu kwa wema Wake na ushirika wenu ninyi watu, na milango iliyo wazi ambayo Bwana ametupa. Na kwa njia ya hawa Wafanyabiashara … Siku zote nimekuwa nikishindania kuwa ni-sikuamini juu ya … Nina imani na watu walio katika madhehebu, lakini sina muda mwingi wa kushawishi madhehebu, kwa sababu kila moja hujizungushia lenyewe uzio, na …

[20] Na ni kama tu ni … Ninaamini ni usemi wa Ndugu mdogo Daudi, juu ya kwamba alikuwa anafuga mabata kiasi fulani, na akasema mto ulikuja na kila bata, unajua, aliyetaka ushirika mmoja kwa mwingine na hawakuweza kufanya hivyo kwa sababu wote walikuwa wamezingirwa na uzio. Lakini maji yalipoongezeka yakafika juu sana yaliwagharikisha mabata toka kwenye kizizi yakawa yanaelea tu.

Hivyo na-nadhani hivyo ndivyo ipasavyo kufanyika. Ni hivyo tu … Maji yanakuja juu (Unaona?), na tunaweza kutoka nje ya hicho kizizi na-na kuwa na ushirika sisi kwa sisi, mnajua, tukawa na upendo halisi wa Kristo mioyoni mwetu.

[21] Na hawa Wafanyabiashara wa Injili Nzima wamekuwa-chemchemi ya raha kwangu, kwa sababu mara nyingi nimekuwa na ndugu, ndugu wazuri, katika, nadhani, kila dhehebu nililowahi kukutana nalo, Wapresbiteri, Lutherani, Babtisti, Wapentekoste, hao-aina zote za Wapentekoste, Kanisa la Mungu, na Wanazareno, Pilgrim Holiness, ndugu wazuri kila mahali … Lakini mara nyingi hawawezi kunipokea mimi katika jumuia yao, kwa sababu … Mnaona? Siyo kwamba hawaamini hili, lakini, tazama hiyo ingewakatilia mbali kutoka kwenye dhehebu lao. Na wakati unapofanya hilo, bila shaka hilo-hilo linatimiza hicho.

Mioyo ya watu inavunjika kwa hofu.

Mjazwe Roho, taa zenu zikiwa zemetengenezwa na zikiwa angani.

Mnajua hilo?

Manabii wa uongo wanadanganya. Wanakana kweli ya Mungu

Tunajua hiyo yote ni kweli; Tunajua? {Sehemu tupu kwenye kanda–Mh]

Nampenda, nampenda

Sababu alinpenda kwanza.

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

[209] Ni wangapi wanaompenda kikweli. Inua mkono wako. Sasa, nakutaka, wakati tukiimba huu tena, ushikane mkono na mtu aliye karibu nawe. Useme, “Mungu akubariki msafiri”. Sisi tu wasafiri. Au sivyo? [Kanisa linasema “Amina–Mh].

Wasafiri na wapitaji

Nampenda

Hilo ndilo lenyewe, hapa hapa upande wa pili wa meza.

Nampenda

Sababu alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari

[210] Je, unapenda kuingia kwenye Unyakuo? (Kusanyiko lasema “Amina”–Mh.) Ni wangapi wanaopenda kuingia kwenye Unyakuo. Useme, “Bwana nataka kuufikia, kwa moyo wangu wote.”

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika, unaujua huo wimbo? Dada unaujua? Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Sijui uko katika nini. Hicho ni kipi? Loo!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Jenga matumaini yako katika mambo ya Milele. Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika.

Unapenda hilo?

Wakati safari yako imekamilika,

hakuchukuliwa kutoka kutoka katika dhebebu, lakini amechukuliwa kutoka katika kifuani mwa Neno la Mungu tulilopewa katika siku hii.

[205] Unyakuo!

Baragumu yake Bwana itapigwa,

Waliolala mauti katika Kristo watafufuka,

Na kushiriki utukufu wa ufufuo wake.

Wakati waliochaguliwa watakusanyika

Kwenda Nyumbani kwao ngambo ya pili ya anga.

Wakati majina yakiitwa ngambo kule, hebu sote hujitahidi kuwepo Pale, marafiki Mungu awabariki.

[206] Limekwishanenwa, sharti litukie. Litakuja kutukia. Na kidog.. [Sehemu tupu kwenye kanda–Mh]

Watu, hakuna hata mmoja aneyetaka kufa-kupotea. Hebu niwaambie chochote ufanyacho …Sijali unakwenda kanisani vema kiasi gani, na umekuwa mwaminifu kwa kiasi gani. Hilo ni jema. Sina neno dhidi ya hilo. Yakupasa uende kanisani. Ufanye hilo. Endelea kuhudhuria tupilia mbali tu mapokeo yako, uingie ndani ya Kristo. Sababu parapanda inakwenda kulia katika moja ya siku hizi, na unakwenda kupatikana ukiwa na alama ya mnyama juu yako, na usijue ni kitu gani hadi uwe umechelewa mno. Hilo ni sahihi kabisa.

[207] Mungu awabariki. Nasikitika kuwa nimewakawiza hivi. Na kumbuka nimewakawiza wao kirefu mno hapa. Hilo ni sahihi. Na sadaka mliyoitoa kwa ajili yangu … Ambayo sikuwaomba mtoe, ndugu. Hilo ni huo ni uungwana. Muichukue na kulipia gharama za hoteli – muda wa ziada tuliokaa, sababu nimekuwa nayo tukitumia. Nilikuwa na mambo machache tu hapa. Nilikwa na kurasa nane au kumi zaidi hapa juu ya Unyakuo pale, lakini si-sikuwa tu na muda kuyaleta hayo. Mungu awabariki.

[208] Je, mnampenda Bwana Yesu? [Kusanyiko lasema “Amina”–Mh.] Hebu tusimame wima kwa dakika moja sasa, kwa kimya kwa heshima, na kumbukeni yale ambayo nimesema. Kumbukeni tupo katika saa za mwisho.

Mataifa haya yanavunjika,

Ishara zile ambazo Biblia ilizitabri.

Siku za Mataifa zinaishia, pamoja na machungu yakilundikana;

“Rejeeni kwa walio wa kwenu enye mliotawanyika”.

Siku ya ukombozi imekaribia.

[22] Hapa si muda mrefu uliopita kulikuwepo na ndugu Mmethodisti aliyenijia. Sitamtaja jina lake, mtu mzuri. Alikuwa anaandika hoja kuhusu Uponyaji wa Kiungu, na alikuja kwangu kwa ajili ya-maongezi kidogo. Tuliketi na kuongea kidogo. Na alisema, “Kitu pekee tulicho nacho dhidi yako unakuwa na Wapentekoste wakati wote.

Nikasema, “Basi hebu Kanisa la Wamethodisti wadhamini mkutano, nitakuja.”

Hilo lilikuwa tofauti. Mnaona? Yeye-yeye alisema, “Vyema, bila shaka, ni-mimi si Kanisa la Methodisti. Mimi ni mmoja pamoja nao tu.”

[23] Nikasema, “Hilo ndilo jambo lenyewe.” Mnaona? “Wao ndio wenyewe, hao Wapentekoste ndio wanaonifungulia milango. (Mnaona?). Hao ndio ninaoweza kuwaendea. Wote watakaonifungulia, mbona, tuko tayari kuingia ndani.

Kama katika Ufunuo sura ya 3 Yeye alisema, “Nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu yeyote atafungua mlango, nitaingia ndani na kula.” Na huyo alikuwa Yesu. Siku zote nilijua huyo alikuwa Kristo. Na Yeye ndiye Neno. Hiyo ni sahihi. Yeye ndiye Neno.

[24] Na hivyo Wafanyabiashara wa Injili Nzima wamekuwa chemchemi ambapo wote tunaweza kukusanyika pamoja. Hakuna makanisa yanayodhamini hili. Wao kwa pamoja, watu kutoka makanisani na tunakusanyika pamoja katika ushirika kote ulimwenguni, kote, kila mahali.

[25] Na nimesaidia kuundwa kwa mafungamano mengi, mengi, mengi ya Wafanyabiashara wa Injili Nzima, duniani kote. Nashukuru kwa nafasi ambayo nimepewa. Ndani pale Wafanyabiashara wataidhamini, na kisha makanisa yote, wana-wanataka kuja kwa vyovyote vile.

Lakini basi kama … Sitaki kamwe kujaribu kumvuta mtu atoke kanisani kwake. Udumu tu kukaa kanisani mwako na usambaze Nuru. Mnaona? Uwe Mkristo wa kweli, mchungaji wako atakufurahia. Mtakatifu halisi, mwaminifu, wa kweli, mtu yeyote amwaminiye Mungu atamfurahia mtu kama huyo. Ndiyo.

[26] Sasa, ninamshukuru ndugu hapa na mke wake na fungamano hili kwa nafasi hii. Naomba fungamano hili likue; naomba baraka za Mungu zije juu yake, na liwe chombo mikononi mwa Mungu kuokoa mamia na mamia ya watu kabla ya kuja kwa Bwana. Na mafungamano yote yaliyosalia-au wawakilishi hapa kutoka mafungamano hayo …

[27] Katika Kitabu cha Zaburi … Sasa ninataka kuhubiri juu ya-ya somo geni kabisa usiku huu, kwa muda mfupi tu. Ninayo Maandiko niliyoandika chini

hapa, na-na niliwaza labda kuwa … Usiku huu nilikuwa ninakwenda kuhubiri juu ya kitu tofauti, lakini tazama wakati unakwenda,, mbona, sikupenda kukaa hapa kirefu namna hiyo, hivyo niliingia hapa na nikapata Maandiko mengi zaidi. Na ninataka kuhubiri juu ya somo la "Unyakuo" Unaona?

[28] Sasa, tunaamini kuwa kutakuwepo unyakuo. Wakristo wote wanaamini hivyo, hao ni wasomaji wa Biblia wanaamini kuwa kutakuwepo na unyakuo.

[29] Na sasa, kusoma kwa ajili ya-kuweka msingi, tunasoma Zaburi ya 25 – Naanisha-samahani-Zaburi ya 27 aya 1 hadi 5.

BWANA ni nuru yangu na wokovu wangu,

Nimwogope nani?

BWANA ni ngome ya uzima wangu,

Nimhofu nani?

Watenda mabaya waliponikaribia,

Wanile nyama yangu,

Watesi wangu na adui zangu,

Walijikwaa wakaanguka.

Jeshi lijapojipanga kupigana nami,

Moyo wangu hautaogopa.

Vita vijaponitokea,

Hata hapo nitatumaini.

Neno moja nimelitaka kwa BWANA,

Nalo ndilo nitakalolitafuta,

Nikae nyumbani mwa Bwana,

Siku zote za maisha yangu,

Niutazam uzuri wa BWANA,

Na kutafakari hekaluni MWAKE

Mradi atanisitiri bandarini MWAKE

Siku ya mabaya,

Atanisitiri katika sitara ya hema yake,

Na kuniinua juu ya mwamba.

Naomba Bwana aongeze baraka Zake katika kule kusomwa kwa Neno Lake.

[201] Na ndipo wakati hao wanawake walipopita pale, wote wakifanya aina zote za dansi la roki na mambo ya aina hiyo, na nywele fupi, na nyuso zilizopakwa marangi. Na walipopita pale namna hiyo, walipaswa kuwa mabikira kwa ajili ya Kristo. Na wakati yeye alipopita pale namna ile, niligeuza kichwa changu, unajua, na jambo hili likiendelea kutendeka mbele yangu. Ilikuwa-migongo yao, ilikuwa inatia aibu. Na ndio hao, wakienda namna hiyo. Na nikageuza kichwa changu, na kulia, namna ile.

[202] Nikasema, "Si-sikuweza kuvumilia hilo ndani pale. Bwana akiwa amesimama pale, na mimi tunajua kuwa mimi mhudumu wa Kanisa, na hicho ndicho nilichoweza kumzalishia Yeye." Nikasema, "Ee Mungu, mimi siwezi kulitazama hilo. Hebu nife. Hebu-hebu mimi nififie," na namna hiyo.

[203] Na pindi tu walipotoka nje, kila wakati mmoja wao alipokuja, wangekwenda nje hadi mahali fulani, ndipo wanadondoka na kuishia. Niliweza kusikia tu sauti yake wakati walipoondoka.

Ndipo nikasikia kitu kama endeleeni mbele askari wa Kikristo. Nilitazama, na hapa kunakuja kile kikundi kitakatifu cha wasichana wadogo, wakiwa namna ile ile walivyokuwa awali, wote wakiwa wamevaa ipasavyo, nywele zao zikining'inia chini mgongoni. Watulivu, wasafi, wakitembea namna hii, kwa hatua za Injili. Msichana huyu alikuwa ndiye Neno. Walionekana kama mmoja kutoka katika kila taifa. Nilikuwa ninatazama hilo walipokuwa wanapita pale, na kuwaona wao wakipita karibu hapo. Badala ya wao kwenda chini, walianza kwenda juu.

Niligundua mmoja wao akijaribu, wawili au watatu miongoni mwao, wakijaribu kutoka nje ya mstari. Nilipaza sauti, "Kaa mstarini." Na maono yakaniacha. Na nilikuwa nimesimama chumbani, nikipaza sauti, "Kaa mstarini." Mstari. Vile.

[204] Ajabu, ingewezekana kuwa tayari umekwishapita? Ingewezekana kuwa Bibi arusi amekwishaitwa? Je hilo ndilo tunaloendelea nalo leo?

Bibi arusi itabidi afinyangwe kuwa na sura Yake Kristo, na Kristo ndiye Neno. Hilo ndilo jambo pekee. Mnaona? Lipo ndani mle, katika Neno. Ni … Mnaona? Hapawezi kuwepo kitu chochote kilichoongezwa. Haiwezekani kuwa ninii mwanamke mwenye mkono mmoja ufananao na wa mwanamume, na mkono mwingine wenye kiganja kinachofanana na uwayo wa mbwa. Inapasa iwe kabisa Neno la Bwana, kama yeye Bwana alivyo Neno. Bibi Arusi ni sehemu ya Bwana Arusi. Mwanamke ni sehemu ya mume wake; kwani ametolewa kutoka katika mwanamume. Hawa alikuwa sehemu ya Adamu toka ubavuni mwake. Na ndivyo ilivyo kwa Bibi Arusi,

194 Sikujua kwamba nilisema haya. Lakini huyu ndugu hapa, naamini alikuwa … Hapana. Mmoja wa akina Mosley, naamini, alinichukua tukaenda nje barabarani kule. Sikujua ni ilikuwa ni kitu gani hadi nilipotazama nyuma. Nilitazama nyuma kwenye Maandiko.

Na Yesu alisema, “Kapernaumu, Kapernaumu, ni mara ngapi … Wewe uliyejiinua, namaanisha, kwenda juu Mbinguni, utashushwa chini hadi kuzimu. Kwani kama matendo makuu yaliyotendwa kwako, yangekuwa yametendwa Sodoma, ingelikuwa imesimama hadi leo.” Na miaka kama mia moja hamsini kutoka pale (Sodoma ilikuwa tayari ndani ya ardhi), ndipo Kapernaumu, nayo, leo imo katika maji.

195 Na Roho yule yule wa Mungu aliyesema mambo haya, na kuyafanya mambo haya yote, alisema pale, “Ee, jiji Kapernaumu, wewe uliyejiita kwa jina la Malaika, Los Angeles jinsi gani ulivyojiinua hadi Mbinguni! Mzizi halisi na makao ya Shetani, mnaona, umejiinua mwenyewe.”

196 Wahubiri, ni makaburini kwa ajili yao. Watu wazuri huenda pale na kufa kama mapanya. Ni vurumai iliyoje!

197 Wewe unayejiita kwa jina la Malaika, kama matendo makuu yaliyotendwa kwako, yangelikuwa yametendwa Sodoma, ingekuwa imesimama hadi leo. Lakini saa yako imewadia.”

Tazameni na muone kama haitakuwa hivyo, mimi ni nabii wa uongo. Mnaona? Jiji lipo hapo. Limekuwa pale.

198 Nakumbuka usiku ule, kabla sijaliona hilo, niliona onyesho la awali la Bibi arusi. Nilisimama pale na nikamwona binti mmoja mdogo, mzuri, amevaa vizuri ipasavyo, na vitu kama hivyo, akitembea namna hii. Kulikuweko na Mtu fulani amesimama karibu nami, katika maono. Na niliona. Wakasema, “Onyesho la awali la Bibi arusi.” Nikamwona Bibi arusi anapita. Wakaja wakapita upande huu, na wakazunguka.

199 Nilisikia akija, ma-makanisa yakija kutoka huo upande mwingine. Likaja pale kanisa la Asia. Ee, ukiongea juu ya uchafu! Likaja hapa kanisa la Ulaya. Loo, jamani! Na ndipo nikasikia rock end roll ikija, na ilikuwa ni Bi Matekani, kanisa, na halikuwa limevaa nguo yoyote. Lilikuwa na makaratasi, kama magazeti, ya kijivujivu, akiwa ameyashikilia mbele yake, akicheza dansi ya rock end roll. Bi Marekani, lile kanisa.

200 Nilisimama pale Uweponi Mwake, nikawaza, “Ee, Mungu, mimi kama mhudumu, hicho ndicho kilicho bora zaidi tulichoweza kufanya? Ee! Ee! Unajua jinsi utakavyojisikia. Ndipo nikawaza, “Mungu nifiche. Kama tu ningeweza kuwa mbali na hapa. Kama yote tuliyoweza kufanya, hicho ndicho tumeweza kuzalisha, kama hicho?”

30 Sasa, leo ninapohubiri juu ya somo hili…. Na sasa, baadhi yenu mnaweza kutofautiana na njia zile ninazopita. Lakini ni wangapi hapa wanaoamini kuwa Biblia inafundisha kutakuwepo na unyakuo wa Kanisa? Ndiyo bwana. Hilo ni sahihi. Hilo ni sahihi, kudakwa na kupelekwa kwa kanisa. Kama u Mmethodist Mbabtist, Mpesbiteriani, au chochote ulicho, Mpentekoste kutakuwepo na kudakwa na kupelewa.

31 Na ninadhani katika kuhubiri si-sijaribu tu kuja juu hapa na kusema kitu ninachofikiria kingewapendeza watu. Sijawahi kuwa na hatia juu ya hilo. Nataka nije juu hapa na kusema kitu kama ninavyojisikia kuongozwa kukisema, ambacho nadhani kingekuwa msaada kwako, kitu ambacho kingeendeleza uzoefu wako katika ushirika na Mungu kama wewe u Mkristo, na kama wewe si Mkristo, likufanye ujionee aibu mwenyewe hata ukawe Mkristo. Na hilo ndilo kusudi la mimi kujaribu siku zote kupanga mawazo yangu yalingane na jinsi Mungu anavyoniongoza.

32 Sasa, tumeonywa, kama katika fundisho hili katika siku za mwisho litadhihakiwa. Kama utapenda … Hebu tu tusome kama kwa dakika moja. Ni katika 2 Petro mlango wa 3. Hebu tusome juu ya hili kwa kitambo kidogo, mlango wa 3 na aya ya 3 na ya 4. Hebu tuone kama hili si sahihi.

Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki,

Wafuatao tamaa zao wenyewe,

Na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?

Kwa maana tangu baba zetu walipolala,

Vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo,

Tangu mwanzo wa kuumbwa.

Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuweko mbingu tangu zamani na nchi pia,

imefanyizwa kutoka katika maji na ndani ya maji,

kwa neno la Mungu.

Kwa hiyo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji ikaangamia.

33 Sasa, tunaona kuwa sababu ya wengi kujaribu kubahatisha kupata ukweli wa somo hili, ni kwa vile nabii hapa alisema kuwa katika siku za mwisho hawa wafanya dhihaka wangekuja wakisema mambo haya. Mnaona ? Limebashiriwa. Sababu ya watu kutenda leo jinsi wanavyotenda ... Mbona, hakika unatarajia hilo, kwa sababu Biblia ilisema hivyo! “ Katika siku za mwisho wangelikuwa wenye kiburi, wenye kujiinua, wapendao anasa kuliko

kumpenda Mungu, wasiotaka suluhu, wasingiziaji, wakali, wanaowadharau walio wema, wenye mfano wa utawa, lakini wakikana nguvu zake, jiepushe na watu wa aina hiyo. Je tutazamie kuigwa kwa ile Kweli? Hakika.

34 Wakati Musa alipokwenda nchini kule Misri kuwakomboa wana wa Israeli akiwa na fimbo tu mkononi kwa ajili ya uthibitisho, Mungu wa mbinguni akiwa nyuma yake, yeye alitenda miujiza. Walikuja waigizaji nyuma yake walifanya kitu kile kile yeye alichofanya. Mnaona ? sasa, walikuja kufuatia nyuma baada ya yeye kutenda kwanza. Ndipo nao wakaja pale, kwa sababu wao walikuwa wananakili kufuatia kile ambacho yeye alitenda, wakiiga lile la asili. Tunalikuta hilo.

Na sasa, unasema, “Vema, hilo lilikuwa ni wakati wa Musa”

Lakini Andiko hilo hilo linasema kuwa watakuja tena katika siku za mwisho, “ Kama Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, ndivyo watakavyofanya hao watu walioharibika akili zao kuhusu ile kweli “Mnaona? Uigaji, kila aina ya mambo ili kuwavuruga watu…

35 Na ndipo, kama unyakuo huu ambao unakuja kutokea… Na chochote kile Mungu alicho nacho katika njia ya Neno Lake, daima kuna mambo fulani yatakayojitokeza ili kuvurunga hilo kama yataweza. Ni-ni-ni kusudio la Shetani kufanya hilo.

36 Kama ndugu huyu hapa kutoka mkutanoni kule Las Vegas alivyosema, “Shetani,” kasema, “ulimwengu ulikuwa milki yake na-na hiyo ikiwa makao makuu yake juu pale.

“Ninajua kuwa Shetani ndiye mungu wa dunia hii. Kila taifa chini ya mbingu linadhibitiwa na yeye. Hivyo ndivyo hasa. Ulimwengu ni wa Shetani. Lakini Yesu atatwaa milki hiyo. Shetani alimtolea Yesu milki hiyo siku moja, na Yeye aliikataa, lakini yeye alisema kwa sababu alijua Yeye angekuwa mrithi wake katika nyakati zijazo.

37 Wenye dhihaka, hebu kwa kitambo kidogo tulichukue hilo neno moja kabla hatujaendelea mbele. Wenye dhihaka …

Nilikuwa ninasoma gazeti moja kama majuma mawili yaliyopita kule Tucson pale ambapo Waingereza fulani kutoka uingereza walikuwa wametoa tamko (ilikuwa katika vichwa vya habari gazetini). Kuwa kusulubiwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo kulikuwa tu bandia kati ya Pilato na Yesu, kuwa Yeye alikuja kujifanya – ili tu kujifanya Mwenyewe kuwa kitu fulani. Na hakuna njia ya sisi kuweza kukanusha hilo kwao, kwa sababu mambo yote ya Mungu hupokelewa kwa imani. Sharti tuamini hilo. Sasa, yeye aliendelea mbele kutoa maelezo jinsi ambavyo hilo lingeliweza kutendwa.

189 Angalia, Isaya, yule kijana mwenye akili nyingi amesimama pale. Ghafla, roho anamgonga. Hakuweza kusema kilicho tofauti. Yeye alikuwa nabii. Yeye alisema “Tazama bikira atachukua mimba”. Maana kwa ajili yetu mwana amezaliwa, Mtoto amezaliwa, tumepewa mwana. Jina lake ataitwa, Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele. Mwisho wa … uweza wa kifalme utakuwa mabegani mwake. Mwisho wa … Utawala wake hautakuwa na mwisho “ Ingewezekanaje kwa mtu huyo kusema kutokana na akili zake kuwa bikira angelichukua mimba?

Kila mtu alitafuta hilo mahali ambapo lingekuwa. Lilikuwa limenewa. Lilikuwa HIVI ASEMA BWANA; Ilikuwa lazima litukie kwani lilikuwa ni Neno la Bwana. Sawa na jinsi ilivyokuwa katika kitabu cha Mwanzo, wakati yeye alipopanda zile mbegu chini ya bahari pale ambapo “palikuwa ukiwa, tena utupu, na maji juu ya kilindi” Mnaona? Ilibidi hilo litimie. Na siku moja, miaka mia nane baadaye, tumbo la uzazi la bikira lilichukua mimba ya mbegu ya Mungu, mbegu iliumbwa. Yeye akamzaa Mwana.

190 Mwana huyo huyo alisimama pale siku moja, Akasema, “Lazaro njoo huku”’ Na mtu aliyekuwa amekufa tangu siku nne, ameoza, pua yake ilikuwa imetumbukia, ananuka, alikuja nje. Kasema:

Msistaajabie hili, kwani saa yaja, amina, wakati wote walio makaburini wataisikia sauti ya

Mwana wa Mungu.

Hivyo, hilo limekwishanenwa Sharti litukie namna hiyo. Kutakuweko na unyakuo. Lo jamani!.

191 Nakumbuka, ule ujumbe wangu wa mwisho tu kule California, ambapo nilidhani kuwa singerudi tena kule kamwe, wakati nilipobashiri, “Los Angeles itazama chini ya bahari HIVI ASEMA BWANA. “Itakuwa hivyo. Huko kumekwisha. Huko kumeoshwa. Huko kumekwisha. Huko kumeoshwa. Huko kumekwishamalizika. Itakuwa saa ngapi? Mimi sijui ni lini, lakini itazamishwa. Baada ya hilo tu matetemeko ya ardhi yameanza kutingisha na kupindisha nchi.

192 Kumbukeni, wengi wenu watu mlikuwa mmesimama pale pale wakati yule Malaika aliposhuka chini pale. Na ule Mwanga wa Moto uliposhuka kutoka Mbinguni, karibu na mwamba hapo tulipokuwa tumesimama pale. Miamba ilivurumishwa toka milimani na kuanguka upande mwingine kule. Kulitokea milipuko mara tatu, mikali. Nikasema, “Hukumu itapiga Pwani ya Magharibi.” Siku mbili baada ya hapo, Alaska karibu ingezama.

193 Kumbuka, Mungu yule yule aliyesema kuwa, “Los Angeles imehukumiwa.” Na imekwisha. Sijui ni lini. Siwezi nikawaambia.

mlima. Kiweko hiki.". Yeye alinena, unaona Alimradi kilitoka kinywani mwake kikiwa Neno, Sharti kidhihirishwe Sharti kiwe. Wakati…

183 Ndipo siku moja aliwaita watu wake wotoke nje. Na alikuwa amemnenea mtu mmoja aliyeitwa Musa, kwa Nguzo ya Moto, Mwanga, Moto Mtakatifu uliowekwa wakfu, na Musa hakuweza … Watu hawakuweza kumwamini Musa, hivyo Yeye akasema, "Walete nje hadi mlima huu".

184 Asubuhi ile, mlima ulijaa moto, na kumulika na ngurumo namna hiyo. Na watu wakasema, "Usimwache Mungu aseme. Hebu Musa aseme unaona, tusije tukaangamia".

185 Mungu akasema, "sitanena tena nao namna hii," lakini nitawainulia nabii. Na nitanena kwa kumtumia yeye, na yale asemayo yatatukia. Basi, lisikieni Hilo, kwa sababu ni-niko pamoja naye". Sasa, yeye alinena hilo. Yeye alisema kuwa hilo litatukia.

186 Mtazame huyu nabii, Isaya, akiwa amesimama pale, mwanamume mtu mwenye akili nyingi, mtu aliyeheshimiwa na Mfalme, kwani alikuwa ameishi na Uzia. Mfalme, aliyekuwa mtu mkuu, alijaribu kuchukua nafasi ya Mhubiri, wakati mmoja na akaingia ndani, akapigwa na ukoma.

Na hicho ndicho nilichowaambia Wafanya biashara. Usijaribu kamwe kuchukua nafasi ya Mhubiri. Hapana, Hapana, bwana. Udumu pale pale ulipo unaona? Ufanye kazi yako, kile Mungu alichoweka, alichokuambia ufanye. Kama wewe u kidole, hutaweza kamwe kuwa sikio! Kama wewe u sikio, hutaweza kamwe kuwa pua, pua au jicho. Mnaona? Kaeni katika nafasi zenu.

187 Mlisikia ule Ujumbe, siku ile nyuingine, katika redio, Kujaribu kumtendea Mungu kazi. Daudi, Mfalme aliyepakwa mafuta. Watu wote wakipiga kelele na kupaza sauti, "Hilo lilikuwa sahihi" Lakini hakutaka ushauri wa nabii. Na mtu mmoja alikufa, na jambo lote likaharibika. Usijaribu kumsaidia Mungu. Usubiri hadi muda wa Mungu ufike. Liache lije katika njia yake ya kutenda hilo. "Nitaanzisha kitu hiki kikubwa kitafanya hivi' Uwe macho, ndugu.

188 Sasa, Daudi alijua vema kuliko hivyo. Nathan alikuwa nchini katika siku hizo. Wala hakutakwa shauri kabisa. Mnaona/ Yeye aliwataka shauri makapiteni wa mamia na maelfu. Watu wote walipiga kelele, na kupaza sauti, na kucheza. Badala ya..Wao walikuwa na msukumo wote wa kidini, lakini haikuwa katika msitari na utaratibu wa Neno la Mungu, na hilo lilishindwa.

Kitu kingine chochote, kisichokuwa katika msitari na utaratibu wa Neno la Mungu kitashindwa. Ni Neno la Mungu pekee litakalodumu milele. "Mbingu na nchi zitapita, lakini siyo Neno Langu.

38 Hapo kitambo kidogo kilichopita katika hilo taifa kuu, London, namaanisha katika Uingereza, pale ambapo John Wesley na Charles na wengi wa wale wahubiri wakuu wa siku za mwanzo, Spurgion na wengineo walikuwa wamehubiri Injili katika masoko ya nyasi kavu na kila mahali kule, waliukataa ule ujumbe wa siku yao na tazama kile walicho katika siku hii.

Hapo ndugu Williams na wengineo walipo usiku huu Imekuwa mojawapo ya nchi zenye hadhi ya chini zaidi ulimweguni. Nimetembea ulimwenguni, lakini sijui mahali pengine palipohitimishwa vibaya kama–kama-kama Uingereza. Ni … Billy Graham alisema kitu hicho hicho. Mbona, ilibidi amuondoe mke wake kutoka kwenye viwanja vya mapumziko, jinsi ambavyo yale yale–yale-matendo ya - yaliyokuwa yakiendelea kati ya wanaume na wanawake hadharani katika viwanja vya mapumziko. Wakati nilipokuwa pale sikuona kamwe kitu chochote kinachoweza kuvunja moyo wa mtu kuliko kile kilichokuwa kinaendelea kule Uingereza, nchi ambayo ilikuwa na nafasi na wakati mmoja iliongoza ulimwengu katika matengenezo ya kanisa. Hiyo inaonyesha tu jinsi iwezavyo kuanguka.

39 Lakini unaona kinachofanya hilo ule ujumbe uliopita wakati huo, Waingereza wanajaribu kuushikilia ujumbe huo huo kwa ajili ya leo. Huo hautafaa leo. Haitawezekana.

40 Ingekuwaje… Ingekuwaje kama Musa angekuwa amekuja na kuleta ujumbe wa Nuhu" Tutajenga safina na kuifanya ielee majini katika mto Nile" ? Isingewezekana. Na wala ujumbe wa Yesu usingefaa kutumiwa na Musa. Na wala ujumbe wa Wesley kamwe hautafanya kazi katika Luther, au ujumbe wa Luther ufanye kwa Wesley.

Na leo, sisi matengenezo yetu ya kanisa ambayo tumekuwa nayo mara ya mwisho yaliyopita kabla ya wakati wetu ilikuwa Upentekoste. Na leo tunaondoka kutoka katika hilo, na ujumbe wa Upentekose hautachanganyika na hili, kwa sababu hii ni siku nyingine. Yote ni Neno la Mungu, lakini ni jengo linaloendelea kujengwa. Kama nyayo, mikono, ikija juu, inamuunda Bibi arusi kwa ajili ya unyakuo mnaona? Usi–Usiwabadilishe watu wa kule nyuma kutoka mahali pao walipowekwa; wao waliishi ujumbe wao.Wao wote wale waliokuwa katika Bibi arusi watainuka kama tu uhai unavyopitia shina la ngano. Unaacha ngano – lile ganda, lakini ile ngano inajiunda yenyewe, kama chembe ya ngano iliyoanguka ardhini.

41 Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa ninasoma kitabu ambacho Mjerumani mmoja, aliandika katika kukosoa, alisema. "Katika wote – katika mashabiki wote wa dini ulimwenguni, William Branham ndiye wa kwanza kwao". Akasema, "Mbona yeye si chochote isipokuwa….Yeye ni - Yeye ni mchawi. Hufanya mambo haya…" Mnaona, huyu mtu bila kujua…

[42] Na ndipo huyu mtu alikuwa mkosoaji, Yeye wala hakumwamini Mungu. Yeye alisema, " Mungu wa aina hiyo ambaye aliweza kuketi katika zile nyakati za zamani za giza, akaweka mikono yake penye kitambi chake, na akichekelea vikundi vya Wakristo wakiwa akina mama, na wanafunzi wake mwenyewe walipasa kuwa mama wenye watoto wachanga na kadhalika na aruhusu simba wawale na Yeye asiweze kamwe kugeuza hata mkono wake". Unaona mahali akili za kimwili zilipo, ambapo elimu na mambo haya haviwezi kudaka maono. [Kusanyiko linasema "Amina"-Mh.]

[43] Ile mbegu ya ngano ilipasa ianguke ardhini kama tu ilivyobidi Yesu afe na kufufuka tena, ndivyo ilivyopasa kanisa la Pentekoste la kale lianguke lilipasa liingie ardhini, ndizo nyakati za giza. Ngano yoyote ambayo – mbegu yoyote inayokwenda chini ardhini, yapasa ilale katika wakati wa giza ndipo ichipue.

Lakini ilianza kuchipua wakati wa Martin Luther, ikaendelea kupitia kwa Wesley, moja kwa moja hadi Pentekoste sasa hadi kwenye – kuendelea hadi kuwa mbegu. Na sasa, ile mifumo ya madhehebu iliyoachwa nyuma, ni mabua. Ndivyo hivyo. Yapasa yachomwe moto, ile mifumo ya dhehebu. Lakini ile chembe halisi ya ngano ambayo ilotokea katika kila moja ya hayo matengenezo ya kanisa itanyakuliwa katika unyakuo wa Bibi Arusi. Wote kwa jumla watafanyika Bibi arusi.

[44] Sasa, tunakuta kule Uingereza pale waliigiza usulubisho si siku nyingi zilizopita, kikundi cha hao watu wenye – watoto wenye nywele ndefu na vitu kama hivyo wakipiga mayowe – wakamuita Yesu" baba" o na vitu vyote hivyo. Mambo duni namna hii!…

[45] Sasa unasema "Hiyo ni London, Uingereza, Tazama yaliyokuwa gazetini hapa Amerika wiki iliyopita. Daktari mmoja mkuu mwenye elimu ya kimungu kutoka shule moja nzuri alisema kuwa – ule usulubisho ulikuwa kitu bandia, kasema kuwa Yesu alijaribu tu kujifanya Mwenyewe kuwa namna ile, kuwa Yesu alikuwa amelewa hili jani la mandraka na hilo… Tunalikuta hilo katika kitabu cha mwanzo hapo linapozungumziwa. Ni gugu kama bangi au kitu kama hicho. Linapatikana katika nchi za mashariki kule. Na kama ukilinywa, litakufanya ulale usingizi, huenda katika - kama mtu uliyekufa, unadondoka siku mbili au tatu kwa matumizi ya mara moja.

[46] Akasema wakati walipompa yeye siki na sifongo, inawezekana kuwa hilo lilikuwa gugu la mandraka. Na walipofanya hivyo walimpa Yeye hilo, na Yeye alikwenda kulewa na kutojielewa kama kwamba alikuwa amekufa. Walimweka kaburini na walimlaza Yeye pale. Baada ya siku mbili au tatu hakika kurejea tena ndipo akaamka tena. Kasema Yeye alikwenda hadi India na akafia mahali fulani huko kifo cha kawaida. Kujaribu kuunda dini bandia.

Upande mwingine alisimama askari wa jeshi la wanamaji, na baharia mmoja upande mwingine. Na palikuwa na ombi lililotolewa. Na upande ule mwingine aliketi mama wa Gold Star. Alikuwa amempoteza mvulana wake. Pale alisimama mke kijana, akiwa amelaza kichwa chake juu ya meza, akilia. Mvulana mmoja aliyevaa nguo zilizotatuka aliketi pembeni, na machozi yakimtiririka usoni. Yeye alikuwa amempoteza baba yake.

Niliwaza, "Ni huzuni iliyoje! Nilisimama hapa na kuangalia, nikawaona askari wachache wa zamani waliobakia, wakitembea chini pale, waliolemaa na kuzeeka, namna hiyo, wakiwa na sare zao, lakini wakizionyesha kwa maringo kwa sababu walikuwa Wamarekani."

Nikawaza, "Ee, Mungu wangu."

[178] Siku moja kutatokea mlipuko kutoka Mbinguni, "Na waliolala mauti katika Kristo watafufuka kwanza." Wale watakatifu wa Agano la Kale nyuma huko, ambao wanasubiri, watatokea kama mlipuko, na watakuja kutoka huko kwanza, na kuingia katika ufufuo. Nasi tutaingia moja kwa moja mstarini, tukielekea angani, miili hii yenye kupatikana na mauti itabadilishwa na kuundwa ifanane na mwili Wake Mwenyewe wa Utukufu. Ni-ni gwaride lililoje litakalokuwa wakati msafara wa kuelekea juu uanzapo, katika baadhi ya siku hizi, katika huo wakati wa kunyakuliwa ulioko mbele, ee wakijivunia kuonyesha Damu ya Yesu Kristo, juu ya vifua vyao, Ujumbe wa Mungu katika saa waliyoishi. Hiyo ndiyo tunayoitazamia, ndugu.

[179] Tazama, katika kufunga tu sasa. Ufufuo wa pili, wote … Kwanza mmoja umekwishapita. Wa pili umewadia, sasa hivi, utadhihirika sasa.

[180] Sasa, wa tatu ni mashahidi wawili wa Ufunuo 11:11 na 12. Ambao, hawa ndio wanaorejea wakiwa na Roho wa Kristo, kuwashuhudia Wayahudi, kama Yusufu alivyofanya kwa ndugu zake. Na kumbuka, "Miili yao iliyokuwa imekufa, ililala barabarani kwa muda wa siku tatu na musu. Kisha roho ya uhai ikawajia, na wakanyakuliwa, wakachukuliwa kwenda juu Mbinguni.

Hizo ndizo Nyakuo tatu za Agano Jipya.

Nyakuo tatu za Agano la Kale, zote zikiwa zimekwishapita.

[181] Sasa, tuko tayari tukisubiri kunyakuliwa, Unyakuo wa watakatifu. Hilo limekwishanenwa, na ndivyo litakavyokuwa. Mungu anaposema jambo lolote, " Mbingu na nchi vyote vitapita, lakini Neno lile halitashindwa kamwe.

[182] Wakati Mungu aliposema nyuma kule katika Mwanzo 1, Yeye alisema "Na iweko Nuru." Ingeweza kupita miaka mamia kabla ya kuweko nuru yoyote. Yeye alisema. "Uweko mtende. Uweko mwaloni, Kuweko jangwa. Uweko

Tazama mwaliko na sauti hapa, ni kitu kile kile wakati wa kurudi kwake. Mnaona?

“Aliitoa roho Yake.” Na alipofanya hivyo, Dhabihu ilikuwa kamilifu, na paradiso ilikuwa tupu. Na watakatifu wa Agano la Kale wakaja duniani tena, wakatembea hapa duniani, na wakaingia pamoja naye katika unyakuo wake.

172 Daudi alisema juu pale, Inukeni enyi malango ya milele, na mwinuliwe” “Aliteka mateka akawapa wanadamu vipawa” na watakatifu wa Agano la Kale wakaingia pamoja naye.

173 Wao walisema “ Ni nani huyu Mfalme wa Haki?.

174 Bwana wa utukufu, mwenye nguvu katika jeshi “Jeshi lenye nguvu hapa wanaingia, wakitembea, “Yesu aliteka mateka”, na huyu hapa anakuja na watakatifu pamoja na watakatifu wa Agano la Kale. Na wakaingia ndani ya malango mapya juu Pale, na kusema, “Fungukeni enyi malango ya milele, na mfunguliwe na hebu Mfalme wa Utukufu aingie”.

Na sauti kutoka humo ndani, ikasema” Mfalme wa Utukufu ni nani”.

175 “Bwana mwenye nguvu vitani.” Malango yakafunguka kwa kasi. “Na Yesu Mshindi akateka mateka na kuwaingiza,” wale waliokuwa wamemwamini Yeye, na Neno lilikuwa limekuja kwao. Pale, Watakatifu wa Agano la Kale wakiwa wamelala pale wakisubiri “Yeye aliteka mateka, akapaa juu”, akawachukua watakatifu wa Agano la Kale na kuingia ndani. Huo ni Unyakuo mmoja, ambao tayari umekwishapita.

176 Unyakuo unaofuata ambao utatukia (Wathesalonike wa Pili) kwa ajili ya Kanisa, Bibi arusi afufuliwe, anyakuliwe aingie Utukufuni. “Sisi tulio hai tutakaosalia,” hiyo ni miili inayobakia duniani, “hatutawatangulia au kuwazuia wale waliolala mauti. Kwani parapanda ya Mungu italia kwanza na waliolala mauti katika Kristo watafufuka.” Mnaona? Na sisi tulio hai tutakaosalia tutanyakuliwa pamoja nao.”

177 Siku nyingine nilikuwa nimesimama penye pembe ya barabara na nikiangalia gwaride la kumbukumbu ya Siku ya Kusimamisha Vita Vikuu, na ilipoelekea juu, kupanda hiyo barabara. Nilisimama pale pamoja na mwanangu mdogo Yusufu. Hapo wakaja wa kwanza, ilikuwa vile vifaru vya zamani vya kwanza vikaja, vifaru vya zamani vidogo. Baada ya hapo vikaja vifaru vikubwa vya Sherman, vya vita vya kisasa, na mizinga mikubwa ikiwa na mitutu yake ya kutolea milipuko-mifuniko ya mitutu juu yake na kadhalika.

Baada ya hapo wakaja askari, wale-wale mama wa Gold Star. Na ndipo kikaja kikosi, na mbele yake kulikuwa na kaburi, “kwa askari asiyejulikana.” Na pale alisimama mlinzi wa lile kaburi.

Kwanza, yule mkosoaji… Watu wana mambo gani ? Mnaona ? Ni siku hii tu tunayoishi wenye dhihaka (Mnaona ?) katika siku hii ili kutimiza unabii

47 Mungu aliligawa Neno lake sehemu sehemu na kugawia kila kipindi sehemu yake. Na kila kimoja cha vipindi hivyo sharti vidhihirishe hilo. Yeye pia alichagua watu kimbele kwa ajili ya kipindi hicho kulidhihirisha kulitimiza lile Neno. Kila wakati alipotoa sehemu ya neno lake, alimweka mtu mmoja kwa ajili ya hilo Neno. Wakati “ Alipotenga wakati wa Musa, Alimtenga Musa pia awe kwa ajili ya wakati huo. Wakati alipotenga muda kwa ajili ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, Alimtenga Yeye kwa ajili ya wakati huo. Kila kipindi amewatenga watu wake, aliwatenga kimbele, kama Biblia ilivyosema siyo chochote ulicho….

48 Kama Mungu hana mwanzo wala mwisho, mwenye nguvu zote, mwenye uwezo wote, aliyepo mahali pote kwa wakati mmoja, ajuaye yote mbona Yeye alijua mambo yote kutoka mwanzoni. Hivyo Yeye alijua.

Hakuna chochote kinachomponyoka, ni sisi tu tunaowaza hivyo? .. kila kitu kinakwenda… Tazama nyuma katika Neno lake na uone kile anachokifanya, ndipo tutakuwa na ufahamu

49 Sasa, fikiria tu. Kwanza kama yule mhudumu angekuwa amefikiria, wakati walipoweka ile siki na sifongo mdomoni mwake, Yeye aliitema. Kwanza yeye hakuinywa (Mnaona?) Ni wenye dhihaka tu wanainuka. Jambo lingine, ilikuwaje Huyu Yesu wa Nazarethi, maisha yake yaliwezaje kuulingana kila unabiii wa Agano la Kale?. Iliwezakanaje?. Isingeliwezekana kama Mungu asingekuwa amepangilia hivyo kimbele. Maisha yake yaliulingana kila unabii wa Agano la Kale. Jambo lingine, kama wale wanafunzi walikuwa wamemfuata kilaghai namna hiyo, kwanini kila mmoja wao alikufa kifo cha mfia dini? Na hata mtume Petro alisema, “Geuza kichwa changu kitazame chini, mimi sistahili kufa kama Yeye alivyokufa. Namna gani. Walimchukua Andrea na kungeuza upande pale msalabani. Kila mmoja wao aliweka ushuhuda wake lakiri ya damu yake mwenyewe. Walimwamini Yeye, na kumpenda Yeye na kumtolea Yeye maisha yao. Kama Yeye alikuwa laghai, Wangewezaje kufanya hayo? Mnaona Huwa watu hawapati matumizi yake ya kiroho.

50 Palikuwepo mtu mmoja mkuu hapa siku si nyingi zilizopita, Rabi mmoja mkuu, ambaye aliandika kuwa Musa alipokuwa anapita katikati ya bahari ya Shamu, kasema, “Haikuwa maji kweli, maji hayakusimama pande mbili kama kuta.” Kasema, kitu kilichotokea ni pale mwisho wa Bahari ya Chumvi palikuwepo matete mengi, naye akapita kati ya maji-matete, matete ya maji. Hayakuweko maji pale, ni matete mengi tu, bahari ya-ya matete ndiyo

waliyovuka. Na makasisi wengi wa kanisa wanaamini hilo-wao na wanalikubali.

[51] Muda si mrefu uliopita hapa wakati yule mwana anga wa kwanza kwenda juu, alirudi na hakuwa ameona chochote cha kumhusu Mungu. Hiyo iliwageuza kimawazo hata wahudumu wengine. Wao walifikiri Mungu aliishi juu pale mahali fulani maili mia moja hamsini kwenda juu.

[52] Mbona, jamani, vipi … Elimu na hekima ya ulimwengu huu imegeuza kanisa kuwa kundi la magugu yaliyovurugika. Wana … Ni …

Elimu, na mifumo ya elimu, sayansi, na ustaarabu ni vya shetani. Ni ustaarabu wa Shetani. Biblia ilisema hivyo. Na ustaarabu wetu ambao unakuja hautakuwa na uhusiano wowote na ustaarabu huu kabisa. Utakuwa ustaarabu tofauti. Katika huu ustaarabu na ulimwengu wa kisayansi huu tulio nao … Sayansi zaidi-tunavyozidi kuwa wa kisayansi, ndivyo tunavyoingia kwenye kina cha kifo, mambo, mitego ya uuaji, na kila kitu. Katika ule ustaarabu mpya hakutakuweko kifo, wala magonjwa, huzuni au hakuna maumivu. Mnaona? Hakutakuweko chochote cha hayo ndani mle. Kwa hiyo huu ustaarabu itabidi uangamizwe, kwa sababu ni wa Shetani.

[53] Tunakuta kuwa katika Mwanzo 4 kuwa watu wa Kaini ndio walioanza ustaarabu, wakajenga miji mikubwa na kadhalika na vyombo vya muziki, na ikawa ni mambo ya sayansi. Na watu wakaenda mbali zaidi na Mungu lakini bado wakiwa wa kidini. Lakini wakati watu wa Sethi walipotokea, walianza ku-kuliitia Jina la Bwana. Aa, kuzungumza kuhusu aliye mwerevu.

[54] Mimi sipo hapa kumtia yeyote uchungu wa moyo, au kusema jambo fulani kuhusu kanisa fulani. Na kama upo hapa na wewe ni wa kanisa hili, sisemi hili kukuudhi, sababu wapo watu wengi wazuri mle kama walivyo katika makanisa mengine. Lakini nilikuwa ninasoma Shriveport wiki iliyopita mahali ambapo kanisa Katoliki lilitoa tamko.

Na tunaona ambapo wote wanaungana sasa penye lile baraza kuu la makanisa na kadhalika wakitimiza tu kile kile Biblia ilichosema wangekifanya, vile vile kabisa.

[55] Sasa tunakuta wao walisema, mbona Biblia, -baadhi ya Waprotestanti wanataka kushikilia isemavyo Biblia. Mbona, kasema, “Biblia si chochote bali ni Kitabu, historia ya Kanisa na hakikuwepo katika hazina ya maandiko ya kale hadi kama miaka mia mbili na hamsini iliyopita. Siku zote limekuwa ni kanisa. Kasema, “Ilikuwa ni kanisa, siyo Biblia, na Biblia ni historia ya yale ambayo kanisa lilifanya. Huo ni uongo wa kierevu ajabu. Mbona tumekuwa na Biblia miaka elfu tatu iliyopita. Agano la Kale limeandikwa katika Maandiko

Wale wengine wakasema, Acha na tuone kama Eliya anakuja na kumuokoa.

Naye Yesu akiisha kupaza sauti…tena kwa nguvu akaitoa…

“Sauti kubwa “Sauti kubwa! Tazama.

Wakati, Yesu, alipokuwa anakufa alipaza sauti kwa nguvu akaitoa roho yake.

Na, tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili, toka juu hata chini, na nchi ikatetemeka, miamba ikapasuka;

Na makaburi yakafunuka, ikainuka miili mingi ... ya watakatifu waliolala,

Nao wakiisha kutoka makaburini, baada ya kufufuka kwake,wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi.

[169] Unyakuo mmoja umekwishapita umetokea mara tatu katika Agano la Kale, wa wale waliokuwa tayari, ambao Neno la Bwana lilikuja kwao. Mnaona? Neno la Bwana lilikuja kwa Eliya. Yeye alikuwa nabii. Mnaona? Neno la Bwana lilikuwa Yesu. Mnaona?

[170] Tazama katika Agano la Kale, wale watakatifu wa Agano la Kale sasa, wakati unyakuo huu wa kwanza ulipotukia. Angalia aya ya 50 sauti yake kuu iliwaamsha watakatifu wa Agano la Kale, kama tu hasa sauti kuu ilivyomwamsha Yesu … au ilivyomwamsha Lazaro. Mnaona? Sauti kuu iliamsha.

Na wa pili unaonekena katika Wathesalonike wa Pili, mlango wa 4. Hebu tu na tusome, tupasome, Tumesoma tu dakika chache zilizopita. Mnaona?

Hatutaki msijue ... ndugu habari zao ... waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama ...

Hiyo ni Wathesalonike wa Kwanza 4:12 hadi 18. Huo–huo utakuwa ni Unyakuo wa pili. Unyakuo wa pili utakuwa ni kudakwa na kuondoka kwa Bibi Arusi.

[171] Watakatifu wa Agano la Kale wamekwishakwenda uweponi Mwake, paradiso imeondolewa. Na watakatifu wa Agano la Kale walipanda juu, kutokana na sauti yake, wakati alipopaza sauti na kuitoa roho yake, kwa sababu (kwa nini?) Dhabihu, upatanisho kwa ajili ya dhambi zao, ambao walikuwa wameungojea, huku wakiamini kuwa yule Mwanakondoo mkamilifu alikuwa anakuja. Walikuwa wametoa dhabihu, wanakondoo. Na wakati alipokufa na kuitoa roho Yake, alipaza sauti yake, na watakatifu wa Agano la Kale wakaamka.

hebu angalia kwa muda mfupi kabla hatujafunga. Tazama. Tumekwishaona hili katika mifano.

166 Sasa, kama unataka kusoma katika Mathayo 18:16, Linasema, wako watatu washuhudiao “unaona, katika Mtakatifu…katika Waraka wa kwanza wa Yohana 5:7, na kadhalika. Tatu daima ni shahidi. Hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, “Amina”–Mh]. Ni thibitisho, kitu ambacho ni sahihi. Mashahidi watatu wanaweka. “Katika vinywa vya mashahidi wawili au watatu, kila neno lithibitishwe.”

167 Sasa tazama. Tumekwishakuwa na mashahidi watatu. Tatu ni ya shahidi, sasa, tumekwishakuwa na unyakuo mara tatu katika Agano la Kale. Je, ulifahamu hilo? Kama shahidi; sasa angalia. Henoko alikuwa mmoja, Eliya alikuwa mwingine, na Yesu alikuwa mwingine.

Yesu, akiwa ndiye aliye muhimu zaidi katika jambo lote sasa Yeye anaweka ushuhuda. Mnaona? Yeye alikuwa ndiye jiwe la kiungo kati ya Agano la Kale na Jipya, kwani ilibidi afe na ndipo unyakuo. Yeye alikufa, akawa hai tena na akatembea hapa pamoja nasi, na ndipo akanyakuliwa kwenda juu. Kwa sababu, yeye alikuwa ndiye jiwe la kiungo lililowafunga hao wawili pamoja. Baada ya Ufufuo wake na unyakuo.. Tazama. Baada ya yeye kufanya hilo, na kuthibitisha hilo, Agano la Kale pale. Sote twafahamu kuwa Henoko alibadilishwa. Tunajua kuwa Eliya alichukuliwa na kimbunga, hilo ni sahihi, akabebwa na gari la Moto. Na Yesu alikufa akazikwa, akafufuka na kuishi hapa duniani, na kisha akanyakuliwa kwenda juu, Yeye Jiwe la Kiungo wako watatu wanaotoa ushuhuda. Hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema “ Amina”– Mh].

168 Sasa pamekwishakuwepo unyakuo mmoja ambao umekushapita tayari mnajua hilo Hilo, hebu tuone kama hatuwezi kulisoma hilo haraka kabisa. Hebu tupate Mathayo, mlango wa 27 . Na hebu tupate aya ya 45 hivi ya Mathayo, mlango wa 27. Hebu tuone kama hatuwezi kupata hilo haraka kabisa na tuone kama –kama hatuwezi kupata kiasi kidogo tu kutokana na hili, lingetusaidia, haraka kabisa. Naamini, 27:45, nimeandika chini hapa. Hebu na tusome

Basi tangu saa sita palikuwa na giza nchi yote hata saa tisa na kama saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema “Eloi Eloi lamasabakthani? Yaani Mungu wangu, Mungu wangu mbona umeniacha?

Na baadhi yao waliohudhuria .. .waliposikia walisema, Huyu anamwita Eliya.

Mara, moja wao akaenda mbio, akatwaa sifongo, akaijaza siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha.

Matakatifu miaka mamia na mamia kabla ya kuja kwa Kristo. Hili jambo la kierevu la Shetani!

56 Na tunakuta katika siku hii wakati wa huku kudhihaki kukuu na kuifanyia Biblia mzaha na kujaribu kuisukumia nje … Yapasa Mungu ahukumu kanisa kwa kitu fulani. Yeye hawezi kuwa tu …

Hawawezi kuja chini barabarani na kunikamata na kusema kuwa ninaendesha mwendo wa maili thelathini kwa saa katika ukanda wa maili ishirini bila ya kuwepo kitu pale cha kuniambia kuwa ninaruhusiwa tu kuendesha mwendo wa maili ishirini. Sharti kiwepo pale.

Na Mungu anakwenda kuhukumu kanisa-anakwenda kuwahukumu watu siku moja. Tunajua hilo. Kuna hukumu inayokuja. Hivyo kama anakwenda kuhukumu kwa kutumia kanisa Katoliki, ni kanisa Katoliki lipi? Kama anakwenda kuhukumu kwa kutumia Methodisti, Babtisti limepotea. Kama atahukumu kwa imani ya umoja, wa imani ya uwili wamepotea. Unaona? Je, anakwenda kuhukumu kwa kutumia nini? Yeye alisema angelihukumu kwa njia ya Kristo, na Kristo ndiye Neno. Hivyo ni Neno la Mungu ndilo Mungu atakalolihukumia. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno. Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili na akakaa miongoni mwetu; Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Unaona? Yeye atalihukumu kwa Neno Lake.

57 Na sasa, tunakuta kwamba katika siku hii, wakati wanapojaribu kusukumia Biblia nje, wakakubali kanisa … Biblia, hawaitaki Hiyo. Kanisa-hivyo wanaweza wakatengeneza kanuni yeyote ya imani au chochote kile na kukiandamia …

58 Vyema, kama nilivyokuwa ninahubiri usiku ule mwingine pale Shriveport. Katika-ushirika, wakati wanapomuua yule mwanakondoo wa sadaka, haikupasa kuwepo “chachu yeyote miongoni mwao, katika kipindi chote cha siku saba,” hapana chachu, hapa mkate uliotiwa chachu. Kila kitu kilipasa kiwe kisichokuwa na chachu. Hilo liliwakilisha vipindi Saba vya kanisa ambavyo tunavipata kitabuni hapa, na hapana chachu. Ni nini? Ni kitu kilichochanganywa na Hilo. Na tunachanganya kanuni ya imani na dhehebu, kila kitu kinginecho, na Neno, na bado tukajaribu kuliita Neno. “Hapana chachu katika kipindi chote cha siku saba.”

59 Na wala kile kinacholiwa leo, usijaribu kukihifadhi kwa ajili ya kesho. “Kiteketeze kwa moto kabla ya mapambazuko,” kwani kuna Ujumbe mpya unaokuja hima, na kitu kipya. Mnaona, wanajaribu kuendelea kukishikilia, lakini huo umekuwa ndio mwenendo wa kanisa. Uamsho unatokea, na jambo

la kwanza utakalojua, katika kipindi cha miaka mitatu, wanauanzishia shirika la dini. Dhehebu linaanza, shirika la dini.

Lakini umetambua? Hili limeendelea mfululizo miaka ishirini sasa, na hapana shirika la dini. Na halitakuwepo kamwe. Huu ndio mwisho. Ngano imejirudia kuwa ngano tena. Ngano imerejea kwenye nafaka Yake. Kapi limejiondoa kutoka Kwake. Na ngano sharti ilale Uweponi mwake Mwana ili iive.

60 Je, si jambo la ajabu kuwa, hivi karibuni, kule Pwani ya Mashariki, kulitokea giza kuu? Wao hawakuweza kulielewa hilo. Wiki iliyopita Texas, ilikumbwa na giza mchana. Hawataweza kuelewa hilo. Je hamtambui kuwa hiyo ni ishara? Je, hamjui kwamba mataifa yanavunjika? Israeli wako nchini mwao nyumbani. Na ishara hizo zinaashiria kuwa tupo mwishoni. Wakati uo huo kunapotokea giza tupu, hamjui ya kwamba hiyo ni ishara ambayo nabii alisema? Naam. “Lakini kutakuwako Nuru panapo majira ya jioni,” kwamba kutakuja kuwepo Nuru itakayokuja wakati wa jioni, wakati vipindi vya giza na mambo kama hayo itakuwa kama ilivyo sasa.

61 Tazama jinsi giza lilivyotokea. Ni wakati uo huo papa alipokuwa amekuja huku.

“Mshirika wa kanisa hili, wakati wao … Mnazo kanda. Nadhani ninyi nyote huwa mnazichukua. Jinsi ile Bwana alivyoonyesha pale siku ile, ndani ya kanisa, kwa ukamilifu mahali ambapo zile nyakati Saba zingekuwa na jinsi ambavyo zingekuwa! Nilikuwa nimezichora ubaoni juu pale, hizo nyakati za kanisa, mnazoziona zimechorwa kitabuni. Na kama Roho Mtakatifu asingekuja chini katika Nguzo ya Moto kubwa, na akaenda nyuma pale ukutani na kuzichora Hizo, Yeye Mwenyewe, hali watu mia tatu au mia nne wameketi, wakitazama hilo!

Na punde tu papa alipoingia hapa, mwezi mahali fulani ulikuwa giza. Na watu walipiga picha zake zikawa kama vile tu zilivyochorwa hapa jukwaani. Sasa amekwishafanya ziara yake hapa tarehe kumi na tatu, akatembea ngazi kumi na tatu, akawashirikisha meza ya Bwana watu kumi na watatu, kwa taifa lililo nambari kumi na tatu, na giza likatokea kila mahali. Je hamwoni mahali tulipo? Tupo wakati wa mwisho.

62 “Wenye kudhihaki watainuka katika siku ya mwisho wakisema, “Hakuna tofauti katika majira haya na jinsi ilivyokuwa, na wakati baba zetu walipolala.”

Lakini uonapo mambo haya yakianza kutukia, inueni vichwa vyenu juu, mmwe tayari. Jambo fulani linaweza kutukia wakati wowote, Kristo akalijia Kanisa Lake.

63 Sasa, hawaliamini hilo, kwa sababu ni … ni … Wao, wame … Wao hawatambui kuwa wao ndio wanaotimiza Maandiko. Watu hakika hawatambui

161 Na tazama, siyo tu Bibi Arusi ameoshwa, amesamehewa, lakini yeye amehesabiwa haki: Mnaona? Je umewahi kwamwe kulichunguza neno kuhesabiwa haki kuona linamanisha nini?

Sasa, kwa mfano, kama ndugu Green alisikia kuwa nilikuwa ninakunywa, nilikuwa ninafanya vitu vibaya ndipo akagundua kuwa sikufanya hayo. Ndipo aje, aseme “Ninakusamehe, Ndugu Branham”.

162 “Unanisamehe? Sikuwahi kufanya kamwe. Unanisamehe kuhusu kitu gani?” Mnaona? Lakini, kama nina hatia basi ninaweza kusamehewa; lakini bado si mwenye haki, kwa sababu nilifanya hilo.

Lakini neno aliyehesabiwa haki ni “kama kwambwa hukuwahi kufanya hilo kamwe.” Aliyehesabiwa haki! Na kisha Damu ya Yesu Kristo hutuosha hivyo kutoka dhambini hata ikawekwa katika Kitabu cha Mungu cha Usahaulifu. Ni yeye pekee awezaye kufanya hilo.

163 Sisi hatuwezi. Tunaweza kusamehe, lakini hatusahau. Ningeweza kukusamehe, lakini siku zote nakumbuka kwamba ulifanya mambo haya maovu. Ndipo, huwi mwenye haki; wewe umesamehewa.

Lakini, usoni pa Mungu, Bibi arusi amehesabiwa haki. Yeye hakuwahi kamwe kufanya hilo kwanza. Amina. Akiwa amesimama pale, akiwa ameolewa na Mwana wa Mungu aliye mwadilifu, hakuwahi kamwe kutenda dhambi, kwanza. Kwanini? Yeye alikusudiwa kimbele. Yeye alitegewa akaingia katika hili. Na sasa wakati aliposikia ile Kweli na akaja kutoka huko, Damu ilimwosha. Na yeye anasimama pale akiwa mwadilifu. Mnaona? Yeye, hakuna dhambi juu yake, kabisa.

164 Hivyo basi, Ujumbe unamwita Bibi arusi akusanyike pamoja unaona, mwaliko.

Na parapanda… Ni yule yule, Yeye mwenye sauti kubwa, yeye alipaza sauti kubwa na ule mwaliko na sauti, na kumwamsha Lazaro. Kwa sauti kuu akisema, Lazaro, njoo huku: Mnaona? Na sauti inaamsha – inamwamsha Bibi Arusi aliyelala, wale waliolala mauti,

165 Na parapanda, “pamoja na sauti ya parapanda” na wakati inapofanya hivyo, inaita. Siku zote, baragumu iliwaita Isaeli waende kwenye sikukuu ya mabaragumu. Mnaona? Ambayo ilikuwa ni Karamu ya kipentekoste, ile Karamu kuu kule angani, na karamu ya mabaragumu. Na, sasa, baragumu ilitangaza kuitwa ili kukusanyika pamoja, “Njooni Karamuni”. Na sasa hiyo ni–ni Karamu ya Mwanakondoo angani.

Sasa, tazama. Kukusanyika pamoja na Bibi arusi, karamu ya mabaragumu, Karamu ya Arusi. Tumekwishaona hili katika mifano. Sasa

Bado kitambo kidogo, ile tingatinga kuu itawasili. Ngano itateketezwa, yale mabua, lakini ngano itakusanywa kwenye ghala Yake. Mnaona?

156 Ninyi si vipofu. Ninyi ni-ninyi ni watu wenye busara. Na kama ningesimama hapa na kusema mambo haya ili kusababisha maudhi? Ninayasema haya kwa sababu ni Uzima, kwa sababu nawajibika kwa Mungu kuyasema. Na ni sharti niliseme, na Ujumbe wangu. Wakati wote, hali nikijua, nyuma kule, chini ya uponyaji na kadhalika namna hiyo, ilikuwa ni ili tu kudaka usikivu wa watu, hali nikijua kuwa Ujumbe ungekuja. Na ndiyo Huu hapa. Na ile mihuri saba imefunguliwa, yale mafumbo na kuonyesha mambo hayo ndiyo kile ambacho kimetendeka. Mimi sikujua hilo.

157 Lakini wako watu waliosimama hapa hapa sasa, waliokuwa wamesimama pamoja nami. Wakati ninyi nyote mlinisikia nikihubiri yale mahubiri: Mabwana, sasa ni saa ngapi? Asubuhi ile, mahali, halisi lilolipo sema lingekuwepo, pale walisimama Malaika saba wakiwa wamesimama pale pale, kutoka Mbinguni. Na walipokuwa wakienda juu, na upepo wa kimbunga ukiwapeleka Wao juu pale, sisi tukiwa tumesimama, tukitazama Wao walipokuwa wakienda zao, sayansi walipiga Hilo picha, njia yote toka mwisho huu wa nchi hadi huu, hata kufika Mexico.

158 Na pale, nilipokuwa natazama, siku moja, nilipoanza kuhubiri hivi Vipindi Saba vya Kanisa. Na nikamwita Jack Moore, mwanatheolojia mkuu. Nikasema, “Jack, ni Nani huyu Mtu aliyesimama pale? ‘Pana Mmoja kama Mwana wa Adamu amesimama pale, nywele zake nyeupe kama sufi.’” Nikasema, “Yeye alikuwa kijana, angewezaje kuwa na nywele nyeupe kama sufi?”

159 Yeye akasema, “Ndugu Branham, huo ulikuwa ni Mwili Wake wa utukufu.” Hilo halikuonekana sahihi.

Lakini nilipokwenda chumbani na kuanza kuomba, Yeye aliniruhusu kuona hilo lilikuwa nini. Mnaona?

160 Nimekuwa nikihubiri siku zote kuwa Yeye alikuwa Mungu, siyo tu mwanadamu. Alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili! Mungu, tabia ya Mungu, ya upendo, tabia kuu zilizoshuka chini, za Mungu, zilizoonyeshwa hapa duniani. Yesu alikuwa upendo wa Mungu, ambao ulijenga mwili ambao Yehova Mwenyenzi aliishi ndani yake. Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu katika mwili. Kile Mungu alichokuwa, Yeye alidhihirisha kwa kupitia huo mwili. Huo mwili ulipasa kufa ili apate kumwosha Bibi arusi na-na-na Damu Yake.

kuwa, wanapofanya mambo haya na kusema, mambo haya, wao wanayatimiza Maandiko.

Ni kidogo kiasi gani Kayafa, kuhani mkuu, na wale makuhani wote wa siku ile, waliomdhihaki na kumfanyia Yeye mizaha, hawakujua kuwa, Mungu Yule Yule waliyekuwa wanamwimba “Mungu wangu mbona Umeniacha? Zaburi ya 22 wametoboa mikono Yangu na miguu Yangu.” Wakiimba hayo hekaluni, na Yeye akifa nje pale msalabani. Hawakujua kuwa walikuwa wanafanya hilo. Hata Yesu aliomba, “Baba wasamehe. Hawajui hilo walitendalo.” Kwa sababu Maandiko hasa yaliwatabiri wangekuwa vipofu.

64 Je ulijua kanisa la Kiprotestanti na Katoliki limetabiriwa, katika siku za mwisho, litakuwa kipofu, kitu kile kile, kwenye Maandiko, Kristo akiwa nje, Akijaribu juingia ndani? Kwa sababu wewe wasema, “Mimi ni tajiri, na sina haja ya chochote’, wala hujui ya kwamba wewe u mwenye mashaka maskini, mnyonge, uchi, na kipofu, na wala hujui hilo.” Ufunuo 3. Ndivyo hivyo, limerudi kwenye upofu tena, likikandamiza vitu vya Mungu, kama kwamba (hivyo) Halikumaanisha chcohcote kwao, wakidhihaki na kulifanyia mzaha. Hicho ndicho Biblia ilichosema.

65 Lakini kwa Kanisa, yule Bibi arusi, Unyakuo ni ufunuo kwake. Hilo limefunuliwa kwake. Huo, huo ufunuo, Bibi arusi wa kweli wa Kristo atakuwa akiusubiri huo ufunuo wa Unyakuo.

66 Sasa, ni ufunuo, kwani ufunuo ni imani. Huwezi ukawa na ufunuo ambao hauwi imani. Imani ni ufunuo, kwa sababu ni kitu kinachofunuliwa kwako, kama ilivyokuwa kwake Abraham, ambaye kitu chochote kilichokuwa kinyume cha jinsi alivyofunuliwa, alikihesabu kuwa hakikuwa hivyo. Sasa, imani, hicho ndicho imani ilicho, ndiyo ufunuo wa Mungu. Kanisa limejengwa juu ya ufunuo, Mwili wote, mzima.

67 Nilikuwa ninaongea hapa wiki chache zilizopita, na mhudumu mmoja wa Kibabtisti. Alikuja huku kujadiliana na mimi. Yeye alisema, “Nimekupenda wewe kama mtu, lakini,” kasema, “ninyi nyote mmechanganyikiwa.”

Nikasema, “Basi naomba unisaidie kunirekebisha.”

Yeye akasema, “Kwa kutumia Maandiko,” akasema, “hatutaweza kamwe, Ndugu Branham, kuyalinganisha mambo pamoja hadi tutakapoweza kulinganisha kila Neno juu ya Neno, juu ya Neno, lilingane kabisa na Kiyunani, na kadhalika.”

68 Nikasema, “Ee bwana, unajua vyema kuliko hivyo.” Nikasema, “Hata katika Baraza la Nikea, huko nyuma mbali kiasi hicho, miaka mia tatu tangu kifo cha Kristo, walikuwa bado wanajadiliana ni yupi msomi wa Kiyunani aliyekuwa sahihi. Unaweza kujua. Jambo lote ni ufunuo. Ni ufu …

Yeye akasema, “Mimi siwezi nikakubali ufunuo.”

Nikasema, “Unawezaje basi kumkubali Kristo?”

Yeye akasema, “Mbona Biblia ilisema, “Yeye aaminiye ame … amwaminiye Yesu Kristo, anao Uzima wa milele.”

[69] Nikasema, “Hilo ni kweli. Hiyo inasema pia kuwa hapana mtu awezaye kumwita Yesu ndiye Kristo isipokuwa kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu aliyemfunulia yeye hilo.” Mnaona? Hivyo ndivyo, unazunguka kurudia pale pale tena, kuangukia nyuma kule kwenye ufunuo. Yapasa liwe limefunuliwa, katika Biblia.

[70] Kaini na Habili hawakuwa na Biblia ya kusoma, lakini ilifunuliwa kwa Habili, kwa imani, ambayo ni ufunuo. Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ile ya Kaini. Ambaye, Mungu alimshuhudia ya kwamba alikuwa mwenye haki.

Wakati Yesu alipouliza hapa, Mathayo 16:17 na 18. hatuna muda wa kulisoma, lakini kama mmeliandika kwenye karatasi. Yeye alisema, “Watu huninena Mimi Mwana Adamu kuwa ni nani?”

Mmoja wao akasema, “Wewe u Musa, Eliya au na kadhalika.”

Yeye akasema, “Lakini ninyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?”

[71] Huyu akasema, “Wewe U Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

[72] Yeye akasema, “Umebarikiwa wewe, Simon, mwana wa Yona, kwani nyama na damu havikukufunulia wewe Hili. Baba yangu aliye Mbinguni Ndiye aliyekufunulia Hili. Juu ya Mwamba huu,” ule ufunuo wa kiroho wa kuwa Mungu ni nani, Yesu ni Nani. Na Yeye ndiye ufunuo wa Mungu, Mungu aliyefanyika mwili na kufunuliwa kwa ulimwengu.

“Yeye alikuwa ulimwenguni. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake, akifunua kile Mungu alichokuwa, katika mwili wa nyama.”

“Wewe ndiwe Kristo, Yule mpakwa Mafuta, Mwana wa Mungu.

[73] Yeye alisema, “Mwili na damu havikukufunulia hili kamwe, lakini Baba Yangu aliye Mbinguni ndiye aliyekufunulia hili. Juu ya Mwamba huu Nitalijenga Kanisa Langu, ufunuo wa Neno kwa majira yake. Nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayatalishinda.”

[74] Kitabu cha Ufunuo ni kitabu cha mwisho cha Biblia. Kimefungwa kwa lakiri kisieleweke kwa wasioamini. Ndani pale Biblia inasema, katika sura ya 22, Yeyote atakayeondoa Neno moja toka Bibliani, au kuongeza kwake neno moja, Nitaondoa sehemu ya huyo kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Basi

[151] Wakati nilipoingia katika mikutano pamoja nanyi, nikiwaombea wagonjwa, hilo lilikuwa jema. Lakini, wakati nijapo na Ujumbe! Kama Ujumbe wowote ukiwaandaa watu, ni Ujumbe wa kweli.

Kama ni miujiza ya Mungu halisi, iliyo ya kweli, na ukaning’inia humo humo katika hilo shirika la dini, unajua hilo halitokani na Mungu, kwani hicho kitu tayari kimekwishatangazwa.

Yesu alipita huko na kuponya wagonjwa, ili kudaka macho yao, hao watu, kisha Ujumbe Wake. Hilo ni sahihi.

Lakini sharti uwe na kitu fulani ambacho Mungu anakwenda kutambulisha. Yeye tu … Uponyaji wa Kiungu, miujiza Yake namna hiyo, ili tu kudaka macho ya watu. Kusudi Lake kuu ni Ujumbe. Hicho ndicho, kile kinachotoka ndani hapa. Yeye anajaribu kupata kukubalika na watu, ili waketi na kumsikiliza Yeye, unaona, kwani wamo baadhi ndani pale waliokusudiwa Uzima.

Baadhi ya nafaka, ngano, zilianguka ardhini, ndege wakazidonoa. Na nyingine zikaanguka kwenye miiba. Na baadhi zilikuwa, zilikwenda katika ardhi iliyoandaliwa, ardhi iliyoandaliwa kabla, na zikazaa.

[152] Sasa,, jambo la kwanza, ni mazingira. Jambo la kwanza ni parapanda na … au sauti … Mwaliko. Na kisha sauti, na ndipo parapanda.

Mwaliko: Mjumbe akiwaandaa watu wawe tayari.

La pili ni sauti ya ufufuo: Sauti ile ile, ambayo sauti kuu katika Yohana Mtakatifu 11:38 – 44, ile iliyomwita Lazaro toka kaburini. Kumkusanya Bibi arusi pamoja; na ndipo ufufuo wa wafu, unaona, kudakwa pamoja Nalo. Sasa tazama mambo matatu yakitukia. Linalofuata ni nini? Ilikuwa ni parapanda. Sauti … Mwaliko, Sauti, parapanda.

[153] Sasa, jambo la tatu ni parapanda ambayo, daima penye sikukuu ya mabaragumu, ni kuwaita watu waende karamuni. Na hiyo itakuwa ni karamu ya Bibi arusi, Karamu ya Mwanakondoo pamoja na Bibi arusi, angani. Mnaona?

[154] Jambo la kwanza linalotokea ni Ujumbe Wake, kuwakusanya Bibi arusi pamoja. Linalofuata ni ufufuo wa Bibi arusi aliyelala mauti, wale-wale waliokwishakufa, huko nyuma katika vipindi vingine, wote wanadakwa pamoja. Na parapanda, karamu huko Mbinguni, angani. Mbona, hicho ndicho kitu kitakachotukia, marafiki.

[155] Tupo pale, tayari sasa. Jambo moja pekee, Kanisa linalotoka nje, lapasa lilale mbele ya Mwana ili liive.

wa uongo” watiwa mafuta, Wanaolijia Neno wakiwa watiwa mafuta wa uongo; waliotiwa mafuta ya kidhehebu, lakini siyo ili kulijia Neno.

Kwani Neno litajishuhudia lenyewe. Halihitaji kitu kingine chochote. Litajishuhudia lenyewe. “Na watatokea watiwa mafuta wa uongo. “ Mnayo kanda yangu niliyohubiri juu ya hilo. Na yule mtiwa….

Aa, ungelimwita mmojawapo, useme. Aaa, wewe Yesu fulani?” “Aa, hakika, hapana”. Hawawezi kusimamia hilo.

[148] Lakini inapofikia pale “Aa utukufu”! Ninao upako. Kumbuka Kayafa alikuwa nao, pia, na akatabiri.

Lakini hilo halihusiani kwa chochote na hili, kwa ndani. Labda iwe kwamba huyo alikuwa mbegu ya Mungu, chembe kutoka mwanzo, Sijali unapiga kelele kiasi gani, unanena kwa lugha kiasi gani, unakimbia, unapiga kelele. Hilo halihusiani chochote na hili.

Gugu laweza kuwa na hali zote mazao mengine yaliyo nayo. Mimi nimeona makafiri wakisimama, na kupiga makelele, na kunena kwa lugha na-na kunywa damu toka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu na kumwitia Shetani. Mnaona? Hivyo usii…Mojawapo ya hisia na vitu kama hivyo, sahau hilo.

Ni moyo wako katika hilo Neno, na huo ni Kristo. Ilete ndani pale, na itazame ikijifanya yenyewe kufahamika, wakati inapofunguka tu kama mbegu nyingine yoyote, na kujitangaza yenyewe katika kipindi inachoishia ndani yake.

[149] Luther hakuleta chochote isipokuwa kitawi. Hawa wengine waliweza hivi vitu vingine. Sasa tupo katika kipindi cha ngano.

Akina Luther wa Luther ilibidi wamlete Luther halisi Pentekoste halisi ilipasa ilete pentekoste halisi. Ndivyo hivyo. Lakini tumekwisha pita kipindi hicho, na tunaendelea mbele.

[150] Unajua, kanisa Katoliki lilipoanza, lilikuwa la Upentekoste? Na kama kanisa la Pentekoste lingedumu kwa miaka elfu mbili lingekuwa katika hali mbaya kuliko Katoliki ilivyo sasa. Hivyo ndivyo hasa. Nawaambia hilo ndugu zangu, dada zangu, ambao ninawapenda. Na Mungu anajua hilo. Lakini kumbuka, marafiki, yanibidi kukutana nanyi ngambo ya pili penye Hukumu. Na hilo huenda lisichukue muda mrefu mno. Yanipasa niwe na ushuhuda wa kile kilicho Kweli.

tunatambua kuwa hicho wamepewa waamini. Na hilo linafungua Kitabu cha Ufunuo na kumfunua Mwandishi wa Kitabu hiki chote ni nani. “Yeye anaonekana kuwa ndiye Alfa na Omega,” kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, Yesu Kristo yule yule tu, moja kwa moja hadi mwisho. Na kinafunua fumbo la Nafsi Yake kikamilifu, na mipango yake kwa ajili ya Vipindi vya Kanisa Lake vilivyokuwa vinafuata, na vikawa vimefungwa ndani pale na Mihuri Saba.

[75] Sasa, Kitabu kiliandikwa, lakini basi, kumbuka, kilifungwa kwa Mihuri Saba. Na hii Mihuri Saba ilikuwa isifunguliwe (Ufunuo 10) hadi kupigwa kwa baragumu ya yule malaika wa mwisho wa duniani akiipiga kwa dunia, Ufunuo 10:7. Mnaona? “Na katika siku za kutangazwa kwa Ujumbe wa malaika wa mwisho, malaika wa saba, siri ya Mungu itakwishamalizika katika kipindi hicho.” Hicho, na hicho ndicho kipindi ambacho tunaishi ndani yake.

[76] Sote tunajua kuwa tunaishi katika Kipindi cha Laodikia. Hapatakuwepo na kipindi kingine baada yake. Haitawezekana. Hivyo tunaishi katika Kipindi cha Laodikia. Na hii Mihuri Saba iliyoshikilia hicho Kitabu ni fumbo kwa watu, yabidi ifunguliwe katika siku hiyo. Hicho ndicho alichoahidi. Sasa, hilo halitakuwa chochote kilicho nje ya Neno, kwa sababu huwezi kuongeza kitu kwa Neno wala kuondoa kitu kutoka kwa Neno hilo. Linapasa kubakia Neno daima. Lakini ufunuo ni kufunua Ukweli kuhusu Hilo, kwamba lenyewe ni nini, kulifanya lilingane na Maandiko mengine yote. Na ndipo Mungu anathibitisha hilo kuwa ndiyo Kweli. Mnaona?

[77] Mungu hahitaji mfasiri. Yeye ni mfasiri Wake Mwenyewe. Yeye hutoa fasiri Yake Mwenyewe kwa kufanya mambo Aliyosema yatatukia yatukie. Kama hapo mwanzo, Yeye alisema, “Na kuweko Nuru,” na ikaweko nuru. Hilo halihitaji mfasiri yeyote. Hilo lilidhihirishwa.

[78] Sasa, Yeye aliahidi mambo fulani katika siku hii ya mwisho, katika Maandiko. Mbona, haya hapa.

Ndiyo Yesu aliyekuwa Mwana wa Mungu. Yeye aliahidi kumtuma. Wakati Yeye alipokuwa katika siku Zake hapa duniani, na watu hawakuweza kumwamini, Yeye alisema, “Chunguzeni Maandiko, kwani mnadhani mnao Uzima wa Milele ndani Yake, na Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Kama sifanyi kazi za Baba Yangu msiniamini. Lakini kama hamwezi kuniamini Mimi, ziaminini kazi nizifanyazo, kwani zinashuhudia kuwa Mimi ni nani.”

[79] Vyema, basi, katika kipindi cha Wesley, kazi alizozifanya zilishuhudia kuwa yeye alikuwa nani.

Katika kipindi cha Luther, wakati wa matengenezo ya kanisa, mbona, hakika ilishuhudia kuwa yeye alikuwa nani.

[80] Katika siku za Wapentekoste, wakati wa kurejesha karama, urejeshwaji wa karama, kunena kwa lugha na kufukuza mashetani, na vile vipawa, mbona hayo yalishuhudia. Hapakuwepo na mzaha kuhusu hilo. Watu walisema, wakati ilipoinuka mara ya kwanza … Nilisoma kitabu cha historia ya Upentekoste. Watu walisema, "Haitadumu kirefu. Itateketea." Bado inaendelea kuwaka. Kwa nini? Ni kwa sababu huwezi ukauzima kamwe. Mungu alisema ungekuwako. Ni sehemu ya hilo Neno, na huwezi ukauzima.

Na ndipo wakati Bibi arusi anapoitwa atoke nje utawezaje kuzima hilo? Ni ufunuo wa udhihirisho wa lile Neno likifanywa kuwa kweli. Na tunaishi katika siku hiyo; Mungu atukuzwe; ufunuo wa fumbo la nafsi Yake.

[81] Sasa, Unyajuo ni tu … Unyakuo huu tunaouzungumzia ni kwa ajili ya Bibi arusi pekee. Kumbuka, Biblia ilisema, "Wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Huu Unyakuo mkuu! Kama hakuna Unyakuo, marafiki, tupo wapi? Tutafanya nini? Tunaishi katika kipindi gani? Tunayo ahadi gani? Kutakuweko na Unyakuo. Biblia inasema utakuweko. Na utakuweko kwa ajili ya wateule, Mke Mteule, Bibi arusi wa siku hii, ambaye ametolewa nje, Kanisa halisi.

[82] Neno lenyewe, *kanisa* linamaanisha "walioitwa kutoka katika." Kama Musa alivyoita taifa litoke kwenye taifa, Roho Mtakatifu anamwita Bibi arusi atoke kwenye kanisa, kanisa litoke kwenye kanisa washirika, kutoka kila dhehebu, wakifanyika kuwa Bibi arusi, mti wa Bibi arusi. Lipo katika-katika kanda, Ule Mti wa Bibi arusi. Bibi arusi akija nje, aitwa, na huyo ndiye aliye huo mti wa Bibi arusi. Ni-namaanisha, Bibi arusi ndiye anayekwenda kuwa katika Unyakuo; hilo tu, hakuna mwingine isipokuwa Bibi arusi, wateule ambao Mungu alitangulia kuwajua tangu mwanzo, nasaba za kiroho za Baba.

Hebu nisimame hapa tu kwa dakika. Na ninaendelea kuwa na wasiwasi, ninapofikiri ninakwenda kuwakawiza, ninakwenda kuwakawiza kitambo kirefu zaidi.

[83] Lakini, angalia, tazama, kila mmoja wenu enyi watu. Je, unajua, miaka kadha kabla hujazaliwa, ulikuwa ndani ya baba yako kama nasaba? [Kusanyiko linasema, "Amina"-Mh.] Hilo ni sahihi. Chembe, mbegu ilikuwa ndani ya baba yako, inatokea kwenye jinsia ya kiume, siyo ya kike. Unaona? Mwili wa kike huandaa yai, kitalu. Lakini ile chembe kutoka kwa ba- … Sasa, tuseme, ndani ya baba yangu …

[84] Au, mwanangu aliyeketi hapa, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, mwanangu alikuwa ndani yangu. Mimi sikumjua, lakini alikuweko. Sasa, kwa kupitia kitalu, kupitia ndoa takatifu, anatokea katika sura yangu. Ninamjua. Ninaweza kuwa na ushirika naye. Na alikuja tu wakati uliokuwa muafaka.

zenu" Na walifanya hivyo. Baadhi yao walikuta hawana mafuta yoyote katika taa zao. Unaona? Lakini ni wakati wa kuzitengeneza taa.

Ni wakati wa Malaki 4. Kile ambacho alia … Ni Luka 17. Ni-ni Isa… Huo unabii wote ambao, Hilo laweza kuweka katika mpangilio wake kikamilifu kwa ajili ya siku hii katika Maandiko, tunaliona hilo likiwa hai pale pale. Hakuna ...

[142] Angalia mambo haya yakitokea ndugu yangu, dada. Wakati, Mungu huko Mbinguni anajua ningeweza nikafia hapa jukwaani sasa hivi. Wewe–ilikubidi utembee tembee kwa kitambo. Ni kwamba tu…. Ni jambo kuu unapomwona Mungu amekuja kutoka Mbinguni, akasimama mbele ya vikundi vya watu, na akasimama pale na kujidhihirisha kama alivyowahi kufanya nyakati nyingine. Na hiyo ndiyo kweli, na Biblia hii ikiwa wazi unaona? Vema. Tupo hapa.

[143] Ta utaratibu wa madhehebu umekufa. Haupo. Hautaamka tena kamwe. Utachomwa moto. Hicho ndicho unachofanya na makapi huko shambani. Kimbia kutoka huko. Ingia ndani ya Kristo, Usiseme, "Mimi ni wa Methodist, Mimi ni wa babtisti, Mimi ni wa pentekoste" ingia ndani ya Kristo.

Kama wewe uko ndani ya Kristo, hakuna Neno lililoandikwa ndani Hapa usiloliamini. Sijali chochote ambacho mtu mwingine yeyote amesema. Na ndipo Mungu anafanya kitu hicho kudhihirisha.Sababu, wewe, wakati Yeye anapomwaga Roho juu ya Neno, kitu gani kinatokea? Kama tu kuweka maji juu ya mbegu nyingine yoyote. Itaishi na itazaa kwa namna yake

[144] Unasema' "Mimi nina ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hivyo haimaanishi kuwa umeokoka, siyo hata kwa mbali.

[145] Tazama hapa. Wewe u kiumbe wa utatu. Ndivyo ulivyo. Ndani katika jamaa huyu hapa pana nafsi, baada ya hapo roho, baada ya hapo mwili. Sasa una hisi tano katika mwili ili kuwasiliana na nyumbani kwako hapa duniani. Hizo haziwasiliani na vinginevyo isipokuwa hivyo. Unazo hisi tano za roho, hapa: upendo, dhamiri na kadhalika, za hiyo, Lakini ndani hapa ndimo unamoishi. Hicho ndicho wewe ulicho.

[146] Je, Yesu hakusema "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki? [Kkusanyiko linasema – "Amina"-Mh.] Uweke gugu nje hapa, na ngano nje pale, na umwagilie zote maji, na uwekee zote mbolea, na vitu kama hivyo, je vyote viwili havitaishi kwa maji yale yale? ["Amina] Hakika. Vema, hicho ni kitu gani? Mojawapo itazaa gugu, kwa sababu hicho ndicho lilicho. Gugu litainua mikono juu na kupiga kelele vile vile kama ngano itakavyofanya.

[147] Je, Biblia haisemi. "Katika siku za mwisho kutotokea Makristo wa uongo [Kusanyiko linasema, Amina"–Mh]. Siyo "Yesu wa uongo", sasa. "Makristo

[136] Sasa, manabii. Kuna kitu kama, " karama ya unabii" katika kanisa, lakini nabii amechaguliwa tangu asili na kuandaliwa kwa ajili ya saa atakayokuwepo. Unaona? Ndiyo, bwana. Sasa, kama unabii unatolewa, wawili au watatu sharti waketi na kuamua kama ulikuwa sahihi au la, kabla kanisa halijaupokea.

[137] Lakini hakuna yeyote aliyeketi mbele ya nabii, kwa sababu yeye alikuwa– alikuwa Neno la Mungu kamili. Alikuwa Neno katika siku yake. Ungemuona Mungu kama katika kioo amedhihirishwa. Sasa, Mungu ameahidi kututumia hilo tena katika siku za mwisho, ili kumtoa Bibi arusi nje ya vurugu ya kidini, katika njia pekee ambayo hili laweza kufanywa.

[138] Haitawezekana kutendeka kamwe, Kanisa haliwezi kumpokea Kristo. Sisi Wapentekoste, hatuwezi kuubeba Ujumbe huu na kuendelea nao katika hali ambayo kanisa limo ndani yake leo. Tutawezaje kuendelea siku za mwisho katika hali ambayo wako ndani yake leo, wakati kila mmoja yuko kinyume cha mwenzake, na kila kitu kingine, na kidini? Aaa rehema ! Ni vurugu imeishia kwenye madhehebu. Na wakati wowote… Na wakati wowote…. Namwalika mwanahistoria yeyote ku-ku- kukosoa hili. Kila wakati ujumbe ulipopita duniani, na wakati walipouundia shirika la dini ulikufa pale pale. Na Upentekoste umefanya kitu kile kile ambacho hao wengine wote walifanya, huu Upentekoste uliokuwa umekuja huku nje.

[139] Ninyi Assemblies of God, wakati Mababa zenu wa kale na mama zenu walipotoka nje ya hayo mashirika ya dini nyuma huko katika lile Baraza Kuu la zamani walipiga kelele na kumsifu Mungu, na walipinga yale mambo. Na mmegeuka kama mbwa kurudia matapishi yake na nguruwe kwenye matope yake" na mmefanya kitu kile kile wengine walichokifanya. Na sasa mmekuwa mno wa taratibu za kidini, na mmefunga mioyo yenu ya huruma. Yakupasa uwe na kadi ya ushirika kabla hujaruhusiwa angalau, kushirikiana nanyi.

[140] Ninyi Oneness, Mungu aliwapa ujumbe kama huo, na badala ya ninyi kuendelea mbele, na kuwa tu wanyenyekevu, na kuendelea mbele, mlilegeza kamba na kujiunda kuwa shirika la dini la kikundi chenu. Sasa nyote mko wapi? Ndoo ile ile.. Ndivyo hivyo kabisa.

Na Roho wa Mungu akiendelea mbel. "Mimi Bwana nimepanda Hili, nitalinyeshea Hili, mchana na usiku. Wengine wasije … Yeye alipangilia kuwa mambo haya yawepo, na ni sharti atume Hili.

[141] Jambo la kwanza linatokea, wakati anapoanza kushuka kutoka Mbinguni, kunakuwepo na mwaliko. Huo ni nini? Ni Ujumbe kuwakusanya watu pamoja. Ujumbe unatokea, kwanza, sasa, ni wakati wa kuzitengeneza taa, "Amkeni mzitengeneze taa zenu". Hilo lilikuwa lindo la ngapi? La saba, sio la sita. La saba "Tazama , Bwana Arusi anakuja Amkeni na mzitengeneze taa

[85] Sasa, ndivyo nawe ulivyokuwa ndani mle, kama unao Uzima wa Milele, ulikuwa … ndani ya Mungu kabla haujaweko ulimwengu. Wewe u sehemu, mwana wa Mungu, zao la Mungu. Yeye alijua hasa kile kipindi ambacho wewe ungekuja. Yeye alikuchagua wewe tangu asili uje kwenye kipindi hicho, uchukue nafasi hiyo, na hakuna mwingine yeyote awezaye kuchukua nafasi hiyo, licha ya uigaji wote na mambo kama hayo. Yakubidi uwepo pale, kwa sababu Yeye alijua kuwa ungalikuwepo pale. Sasa wewe umedhihirishwa. Sasa unaweza kuwa na ushirika Naye, na hicho ndicho anachotaka. Yeye anatamani ushirika, kuabudiwa. Kama maisha yako hayakuwa … daima tunda katika Mungu, wewe u mwigaji tu wa Ukristo. Unaona? Kutakuweko na mamilioni na mabilioni wa namna hiyo, watakuwa waigaji tu wa Ukristo.

[86] Kuna tamshi nililolitoa hivi karibuni. Nilikuwa ninamwangalia kwa makini Ndugu Demos Shakaria pale, wakati walipokuwa na uchanganyaji wa mbegu za ng'ombe, nikaangalia mirija ya kujaribia, na kadhalika, ilivyokuwa ikiingizwa ndani na madaktari, na nikaangalia mambo haya kwa makini.

[87] Katika utoaji halisi wa mbegu za kiume kuna kama milioni zinazotoka kwa dume kila wakati mmoja. Na kitu kama mayai milioni yanatoka kwa jike wakati huo-huo mmoja. Je, ulijua, katika hivyo vimbegu vidogo vidogo vinavyotembea hapo, zikiwa milioni, ni moja tu miongoni mwake iliyokusudiwa uzima, na ni yai moja tu lenye kutungisha mimba? Na kile kimbegu kidogo kitatambaa moja kwa moja kuipita kila moja katika hizo mbegu ndogo nyingine, moja kwa moja juu ya kila kijimbegu kidogo kinachofanana na hiki, na kupita juu ya kile na kuja juu hapa, na kukuta lile yai lililo tayari kutungisha mimba na kutambaa na kupenya ndani yake. Na ndipo hivyo vimbegu vingine vyote hufa. Mbona, ukizungumza juu ya uzazi wa bikira, ee, fumbo hilo halijafikia nusu ya lile la uzazi wa kawaida, jinsi ulivyokusudiwa kimbele, kuchaguliwa na Mungu tangu asili!

[88] Sasa, kule mwanzo, nyuma kule, miaka mingi iliyopita, kabla ya kuanza kwa wakati, wewe kama u Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, usiku huu, ulikuwa ndani ya Mungu wakati huo, Baba yako. Ndiyo sababu, ulipoingia katika maisha haya hapa na ukaukiri Ukristo, vyema, kila kitu kikienda vibaya, ukashangaa juu ya hilo. Lakini, siku moja, Kitu fulani kilikugonga. Kilikuwa kitu gani? Ule Uzima ule uliokuwa chini pale, tangu mwanzo. Na kam ili …

[89] Kama ile hadithi yangu ndogo kumhusu tai, akiikuta, mama alipomkuta huyo tai. Umekwishanisikia nikihubiri juu ya hilo, jinsi yule tai mdogo alivyoanguliwa chini ya kuku. Lakini yule, tabia zake za kujaribu kuwalisha hao-hao kuku, yule tai mdogo hakuweza kulikubali hilo, kwa sababu yeye kwanza hakuwa kuku. Bado alikuwa kwenye banda pamoja na kuku na akawafuata kuku. Lakini mama kuku aliweza kuparura kwenye eneo la

shamba lililozungukwa na nyumba na mambo kama hayo, na yule tai mdogo hakuweza kuvumilia hayo. Lakini kila wakati alipopiga kidoko na kila kitu vile vifaranga vyote huenda, hivyo huyu tai naye alikwenda pia. Lakini siku moja …

[90] Mama yake akijua kwamba yeye alikuwa ameatamia mayai mawili, siyo moja. Ilibidi liwepo lingine moja, mahali fulani. Tai mama alikwenda kuliwinda, akipaa kuzunguka kila mahali akiruka mwendo wa duara. Hatimaye aliruka juu ya eneo la shamba lililozungukwa na nyumba, na akampata mtoto wake, na akampigia yowe. Ilikuwa ni sauti, ambayo kwayo alitambua kuwa hicho ndicho kitu kinachostahili. Hicho ndicho kitu alichokuwa anakitafuta, unaona, na ndipo alipotambua kuwa yeye hakuwa kuku. Yeye alikuwa tai.

Na hiyo ndiyo njia kwa kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, wakati unapokuja. Sijali ulijiunga na madhehebu mangapi, ni majina mangapi, uliweka jina lako kwenye vitabu, na mambo kama hayo. Wakati lile Neno halisi la Mungu linapothibitishwa na kufanyika kweli halisi mbele yako namna hiyo, unatambua wewe u tai papo hapo. Kwa sababu huku kupiga kidoko kote kwa kuku, “Wewe ujiunge na hili na jiunge na hili, na uende njia hii na njia ile,” huo ni upuzi. Ni kule kuongeza Neno kwa Neno kuliko halisi.

[91] Wakati mbegu inapoingia katika tumbo la uzazi la-la mwanamke, haichukui … Hu, hufanyika kuwa mbegu kutoka kwa baba yako, na kisha kinachofuata ukafanyika mbegu kutoka kwa mbwa, na kinachofuata kutoka kwa paka, kinachofuata kutoka kwa kuku. Ilikuwa tu mbegu ya kibinadamu.

Na Mwili wa Yesu Kristo, Bibi arusi, atakuwa sehemu ya Mwili Wake. Ambao uta … Yeye alikuwa lile Neno, na Bibi arusi itabidi awe lile Neno; Neno lililoongezwa kwa Neno. Kuhesabiwa haki kwa Luther, Utakaso wa Wesley, Ubatizo wa Roho Mtakatifu wa Upentekoste, kurejeshwa kwa vipawa, na yote yaliyosalia ya Hilo, yote yanafuatana pamoja na Hili. Mnaona? Haina budi kuwa Neno juu ya Neno, mbegu juu ya mbegu, Uzima juu ya Uzima, kusababisha kuonekana kwa kimo kikamilifu cha Bibi arussi wa Bwana Yesu Kristo. Sasa, kumbuka wewe ulikuwa zao.

[92] Na sasa, jambo lenyewe kuhusu hilo ni, baada ya kufahamu mambo haya, kwamba Kristo anakuja kwa ajili ya Bibi arusi Wake, sasa tunaingiaje ndani ya huyo Bibi arusi? Hilo ndilo swali.

Wengi husema, “Jiunge na shirika letu la dini.” Mmoja wao anahitaji ubatizo wa namna fulani. Mwingine anataka kufanya hili au lile. Mmoja alisema, “Sharti unene kwa lugha, la sivyo hujakipata Hicho.” Mwingine alisema, “Si lazima unene kwa lugha.” Huyu hapa anasema, “Sharti ucheze

Mwaliko, mwaliko ni nini? Ni ujumbe unaopita, kwanza, mkate wa Uzima ukimleta Bibi arusi.

[131] Sasa, Mungu anayo njia ya kutenda mambo. Na Yeye habadilishi utaratibu Wake kamwe. Yeye huwa habadilishi uta … Yeye ni Mungu asiyebadilika. Katika Amosi 3:7, Yeye alisema, “Asingefanya jambo lolote duniani hadi kwanza awafunulie watumishi Wake hao manabii. “Na kama ilivyo hakika tu kwamba Yeye aliahidi hilo, Yeye atalifanya.

[132] Sasa tumekuishapita vipindi saba vya kanisa. Lakini tumeahidiwa katika siku za mwisho, kufuatana na Malaki 4, kuwa kungekuweko na kurejea tena kwa nabii katika nchi. Hilo ni sahihi. Tazama asili yake, yeye angekuwa wa namna gani. Yeye daima…

Mungu anaitumia roho hiyo mara tano: kwanza ndani ya Eliya ndani ya Elisha, katika Yohana Mbatizaji, kuliita kanisa litoke na mabaki ya Wayahudi. Mara tano “neema” Y-e-s-u, I-m-a-n-i na hivyo ni hesabu ya neema. Mnaona? Vyema.

[133] Sasa, kumbuka, Ujumbe umeahidiwa. Na mafumbo haya yote yaliyokuwa yamefungwa matita matita na mafungamano ya kidini itahitaji – nabii moja kwa moja toka kwa Mungu afunue hili. Na hilo ndilo hasa yeye aliloahidi kufanya. Mnaona?

[134] Sasa kumbuka “Neno la Bwana huja kwa nabii,” siyo kwa Mwanatheolojia. Nabii ni picha ya Neno la Mungu katika kioo. Yeye hawezi kusema chochote; hawezi kusema mawazo yake mwenyewe. Yeye ataweza tu kusema kile ambacho Mungu hufunua. Hata kwa yule nabii Balaamu alipojaribiwa ili auzwe, auze haki yake, yeye alisema; “Nabii yoyote awezaje kusema chochote isipokuwa kile ambacho Mungu aweka kinywani mwake? Ni kitu ambacho huwezi kusema kitu kingine chochote. Na umezaliwa kuwa hivyo. Si zaidi ya ambavyo unge

[135] Kama ungeweza kusema, “Ni-ni-siwezi kufungua macho yangu,” wakati unatazama. Mnaona? Huwezi , huwezi kunyosha mkono wako, wakati unaweza. Mnaona? Huwezi ukawa mbwa wakati wewe u binadamu. Mnaona? Wewe umeumbwa tu uwe hivi. Na Mungu pia, kila wakati katika vipindi, kwa njia ya Isaya, Yeremia na wote, Eliya, katika vipindi vilivyopita. Wakati kikundi cha kidini kingefanya kila kitu kiwe vurugu, yeye angemtuma nabii, amwinue kutoka mahali pasipojulikana. Yeye hakuwa mmoja wa taratibu zao, na alinena Neno Lake. Waliitwa watoke kutoka maisha haya na wakawa wamekwenda kabisa, watu wa kweli ya Mungu tu, wasiokuwa na taratibu. Na daima hiyo ndiyo iliyokuwa njia ya kumtambua yeye. Yeye alisema, “ Kama yupo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho au nabii…”

ya saa kumi na mbili na saa moja … au saa kumi na mbili na saa tatu asubuhi fulani. “Kwani baragumu ya Bwana italia.”

Katika asubuhi ile yenye kung’aa na isiyo na mawingu wakati wafu katika Kristo watakapofufuka,

Na washiriki utukufu wa ufufuo wake;

Wakati wateule Wake watakapokusanyika manyumbani kwao mbele kupita anga,

Wakati majina yakiitwa juu huko, mimi nitakuwako.

[128] Neno Unyakuo, wala halijatumiwa kabisa, katika Biblia. Tumeliweka tu hilo neno pale. Biblia inasema, “nyanyuka, kunyanyuliwa juu.” Tunasoma hapa katika Wathesalonike wa Pili … Au Wathesalonike wa Kwanza, ni utaratibu wa huu Unyakuo mkuu utakaotukia katika siku za mwisho. Sikiliza hili hapa. Tunakwenda kuanza hapa na aya ya 13.

Sitaki msijue, ndugu, habari za hao waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama na hao wengine wasio na matumaini.

Maana ikiwa tunaamini … Kristo alikufa na akafufuka, vivyo hivyo na hao … waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja Naye.

*Kwa kuwa twawaambieni haya kwa Neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai tutakaosalia hata wakati wa kuja Kwake Bwana, hatutawantangulia … (*Neno hilo tangulia lamaanisha “kucheleweshe”) … *wale waliokwisha kulala mauti.*

Kwa sababu Bwana Mwenyewe atashuka …

Sasa sikiliza kwa makini.

Bwana Mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na … parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza …

[129] Nawataka mwone jambo kubwa ambalo linatukia hapa sasa. Usilikose hili. Mnaona? Sasa tazama Neno linasema hapa, katika Wathesalonike wa Pili, kuwa kuna mambo matatu ambayo yabidi kutukia kabla Bwana Mwenyewe hajajitokeza. Haraka sasa ili tuweze kufunga. Mnaona? Jambo la kwanza linatokea … Tazama: mwaliko, sauti, parapanda. Hebu tusome sasa na tuone kama hilo ni sahihi. Mnaona?

*Kwa sababu Bwana Mwenyewe (*aya ya 16) *atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu na … parapanda ya Mungu …*

[130] Mambo matatu yanatukia. Sauti … mwaliko, sauti, parapanda, sharti yatukie kabla Yesu hajajitokeza. Sasa Mwaliko … Yesu anayafanya yote matatu wakate Yeye-Yeye-Yeye anaposhuka.

katika roho.” Huyu anasema, “Ni lazima upige kelele.” Huyu, “Nimepata msisimko.” Hilo ni jema, na ndipo bado, lote hilo ni makosa.

Yawezekanaje mtu ambaye … au mwanamke au mtoto wa Mungu, ambaye amezaliwa kutokana na Roho wa Mungu alikane Neno la Mungu? Wakati, Mungu Mwenyewe analifasiri na kusema, “Hili Ndilo Lenyewe, niliahidi Hili. Ndilo Hili hapa.” Akilionyesha Hili katika uwazi kadri iwezekanavyo. Mbona, wamewekewa kuliona Hili. Mnaona? Je, Kristo angewezaje kulikana Neno Lake Mwenyewe? Na kama Kristo yupo ndani yako, hawezi kulikana Neno Lake Mwenyewe.

[93] Tunaingiaje basi katika Mwili huu? Wakorintho wa kwanza 12, “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuingizwa katika Mwili huu, kwa njia ya ubatizo mmoja wa Roho Mtakatifu.” Hilo kama unataka kuliandika ni Wakorintho wa kwanza 12:13. “Kwa maana kwa Roho mmoja sisi sote tulibatizwa.” Na Roho Ndiye Uzima wa Kristo, Hilo ni sahihi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”-Mh.] Uzima wa Kristo! Na uzima wa mbegu yeyote … ambapo Yeye alikuwa ile Mbegu Neno, anaihuisha, ile Mbegu. Je, unalipata hilo? Kama ule … Kama ule Uzima umo ndani ya Mbegu, na huu ubatizo wa Roho Mtakatifu unakuja juu Yake, haina budi kuleta Uzima wa ile Mbegu.

[94] Kama nilivyowaambia, hapa Phoenix kitambo kidogo kilichopita, nilikuwa ninaongea na Ndugu John Sharrit. Nilikuwa nje pale, na akanionyesha mti, mchungwa. Ame-amezalisha matunda mengi. Na alinionyesha mti mmoja, ulikuwa umezaa aina nane au tisa za matunda. Na mimi nikasema, “Ndugu Sharrit, huo mti ni wa aina gani?”

Kasema, “Mchungwa.”

Nikasema, “Mbona limao, na chenza na danzi na balungi?”

Yeye akasema, “Yote ni matunda ya jamaa moja. Vitawi vya miti hiyo yote vimepandikizwa kwenye huo mchungwa.”

Nikasema, “Ah” Kumbe. Sasa, mwaka ujao mti wote utakuwa ni machungwa, kwa …

[95] “Ah, hapana. Kila mti utazaa kwa aina yake. Kila tawi litazaa kwa aina yake.”

[96] Wengi wenu wakulima wa matunda mnajua hilo, hapa katika hili bonde lenye miti ya matunda ya jamaa ya michungwa. Kila moja itazaa kwa aina yake. Ukiweka tawi la mlimao katika mchungwa, litazaa malimao katika mchungwa, litazaa malimao, kwani lina asili moja na mchungwa. Hata hivyo halitazaa tunda lile la asili.

Na ndicho kitu tulichokifanya. Tumepandikiza. Tumeingiza mapokeo, na kadhalika na kupandikiza katika kila moja Hapa. Itawezekanaje Wamethodisti wazae kinginecho isipokuwa mtoto wa Kimethodisti? Itawezekanaje dhehebu lizae kinginecho chote isipokuwa mtoto wa kidhehebu?

97 Lakini kama ule mchungwa utakuja kamwe kuchipua tawi la asili, hilo litazaa machungwa.

Na ndipo basi kama Mungu kamwe atafanya kitu katika Kanisa, kitakuwa cha asili, litarejea lile Neno tena. Kabisa. Sharti iwe hivyo, kwani Uzima umo ndani ya Mti. Nao huzaa kwa aina Yake Yenyewe.

98 Sasa, tunakuta, sasa, kuna lile kanisa kubwa ambalo limepitia katika vipindi vyote, likizaa tunda lake. Na matawi yanapoondoka, wanayakata ili kuyapunguza. Katika Injili ya Yohana 15, hakuukata mzabibu, sasa, Yeye aliyaondolea mbali matawi, aliyakatilia mbali kwa sababu hayakuwa yanazaa tunda lolote. Na-na tuna …

99 Yesu anataka tunatoka kwake, kwa ajili Yake Mwenyewe. Mke Wake sharti azae watoto wa aina aliyo Yeye.

Basi, kama hazai watoto, watoto wa Bibi arusi, Watoto wa Kineno, basi huyo ni mtoto wa kidhehebu. Basi, amerejea wapenzi wake wa kwanza, ulimwengu na dhehebu. Na hawezi kuzaa Mkristo hasa, halisi, aliyezaliwa mara ya pili, kwani hakuna kitu pale cha kuzalisha Hilo.

100 Kama tu ungechukua tawi la mlimao na kulipandikiza pale, litazaa limao, lakini haliwezi likazaa chungwa, kwa sababu halikwepo pale tangu mwanzo. Lakini ilikuwa imekusudiwa hivyo tangu mwanzo, kujua kwa Mungu kimbele, kuchaguliwa tangu asili na kazaliwa, ilibidi izae chungwa. Haliwezi kuzaa kitu kingine chochote.

101 Hivyo ndivyo ilivyo kuhusu Kanisa la Mungu aliye hai, wakati saa inapowadia. Kila mtu … Umwache Mungu aanze kufanya jambo fulani kila mtu anaanzisha jambo fulani na kuendelea nalo. Mnaona? Imekuwa hivyo kila wakati.

Nilikuwa ninasoma katika historia, ya Martin Luther, hapa si muda mrefu uliopita. Alisema, “Hali … Haikuwa vigumu kuamini kuwa Martin Luther angeliweza kuliasi Kanisa Katoliki, kwa mafanikio. Lakini, “kasema,” jambo la kushangaza ni jinsi alivyoweza kushikilia msimamo wake kwa uthabiti juu ya ulokole uliokithiri ulioambatana na uamsho wake, na bado akadumu moja kwa moja kwenye kuhesabiwa haki kwake’” Mnaona? Ni kila kitu tu, uigaji na kila kitu, maanguko.

121 Watazame wanaume wetu. Wanang’ang’ania mapokeo madogo ya dhehebu badala ya Neno la Mungu. Wanang’ang’ania hicho badala ya kutoka nje wakati wanapomwona Mungu amejiweka Mwenyewe kufahamika kikamilifu. Sababu yenyewe, wao ni vipofu. Hawawezi wakiliona Hilo. Hawataliona Hilo kamwe.

Sasa angalia kitu kinachotokea hapa katika hili, hali tunaharakisha.

Nadhani yule bibiye anataka tuondoke. Nimemwona akiashiria mkono wake, kitu kama hicho juu ya kwamba anataka tutoke nje, hivyo ni bora tuharakishe.

122 Sasa basi mtazame Henoko, mfano wa Kanisa. Hapa yeye pia amekuwa mfano wa kipindi cha saba cha kanisa. Je waweza kuwazia hilo? Kipindi cha saba cha kanisa! Tazama , “Wakati wa kupigwa kwa baragumu’” …

123 Ni wangapi wanaoamini kumekuweko na wajumbe saba kwa ajili ya vipindi saba vya kani … Aaa sote tunaamini hilo, kama tunaamini Biblia. Kama hatuamini Biblia, ndiyo kusema, unaona, hatuamini hilo. Lakini wamekuweko.

124 Sasa tunaishi katika kipindi cha Saba cha kanisa. Na wakati Biblia iliposema hivyo, hiki kipindi cha saba cha kanisa, “Wakati mjumbe wa kipindi cha saba cha kanisa aanzapo kuhubiri Ujumbe wake kuwa siri za mambo yote yaliyokuwa yamesokotwa, wakati wote wa vipindi vya kanisa, yangefunuliwa yote wakati huo.” Hapa tunaliona hilo, Mwana Adamu akija miongoni mwa watu Wake na kufanya yale yale hasa, akithibitisha ujumbe Wake kama Yeye alivyosema kuwa angefanya. Hapa tunalikuta hilo kipindi hiki cha mwisho sasa.

125 Na yale malindo saba, kama lindo la saba, linapowadia. Yeye hakuja katika lindo la kwanza, la pili, la tatu, la nne, lakini amekuja katika lindo la saba. Huyo alikuwa ni Henoko, yule wa saba, ambaye alibadilishwa. Na Nuhu akiwa mfano wa masalia ya Wayahudi, watapitishwa kuvuka hapo. Sasa, katika nyakati za Biblia, tukizungumza juu ya yale malindo. Na nyakati za usiku hazikuwa zimegawanywa kwenye masaa, katika nyakati za Biblia.

126 Sasa sikiliza kwa makini. Hivyo nitaharakisha sasa, kwa sababu wanakihitaji chumba hiki. Hapana. Biblia haikuwa imegawanywa, au-au …

127 Usiku haukuwa unagawanywa katika masaa, katika nyakati za Biblia. Ulikuwa unagawanywa katika malindo. Kulikuweko na malindo matatu. Lindo la kwanza lilianza saa tatu hadi saa sita. Lindo la pili lilianzia saa sita hadi saa tisa. Na lindo la tatu la usiku lilihesabika tangu saa tisa hadi saa kumi na mbili. Sasa tuna tatu, tatu mara tatu ambayo ni tisa, nambari isiyo timilifu. Ndipo tunarejea hesabu ya saba kwa ajili ya Unyakuo, ambao utatokea naamini, kati

Inaendelea hivyo! Hivyo ndivyo ambavyo kila kipindi kimefanya. Haiwezekani kabisa kwenda kinyume cha asili. Ni … Huo ni mwendelezo wa Mungu, jinsi ambavyo Yeye anatenda mambo.

[117] Na sasa hicho ndicho kipindi ambacho sisi tunaishi sasa hivi, kipindi cha saba cha kanisa. Sasa yote yatadhihirishwa katika nafaka ya ngano hapo mwishoni, kurejea mwanzo tena. Sasa, kama ukichukua Luka mlango wa 17 na aya ya 30, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma , ndivyo itakavyokuwa katika kuja Mwana wa Adamu, wakati Mwana Adamu aanzapo kujifunua Mwenyewe.” Je, kufunua ni nini? Kufanya ufunuo Wake wa kile Yeye alicho katika siku hii. Wafunulie watu, lile Neno ambalo watu wanajulishwa katika siku hii. Wafunulie watu, kwa udhihirisho wa Roho Mtakatifu kufanya Yesu aishi miongoni mwetu. Na, kumbuka, Yeye aliwakilishwa pale ndani ya mtu. Mtu! Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa” … Sasa, Yeye alisoma Biblia hii hii tunayosoma, Kitabu cha Mwanzo. Sasa, tunaona katika ule mlango wa Mwanzo pale, wakati Yesu alipokuwa anazungumza kuhusu hilo.

[118] Tunaona pale, kuwa katika hilo, hali Yeye akiwa amelipa hema kisogo, na Sara akiwa katika hema. Yeye alisema, Yeye aliuliza swali. Na Sara hakuamini kuwa kile ambacho kilikuwa kinakwenda kutendeka kingewezekana kutendeka. Yeye alisema, “Sasa Abraham, nitakurudia wakati uu huu mwakani.” Mnaona? Na Sara kule hemani, alicheka juu ya hilo. Yeye akasema, Kwa nini Sara amecheka, kule hemani, akisema, ‘mambo haya yatawezekanaje?’”

[119] Yesu aliahidi. Na Huyo alikuwa ni Yeye. Abrahamu alimwita Yeye “Elohim,” Mwenyenzi. Huyo alikuwa ni Yeye. Sasa, Biblia inabashiri kuwa hilo litarejea tena katika siku za mwisho, Yesu alisema hivyo. “Na wakati myaonapo haya mambo yakianza kutukia,” kumbukeni tu, wakati haya yakianza kutukia namna ile, ndipo, hivyo, “tambueni ya kuwa wakati u karibu mlangoni.”

[120] Utazame ulimwengu wenyewe. Utazame ulimwengu. Sodoma, kama Sodoma iliwahi kuweko. Watazame watu walivyopotoka katika upotovu wa namna hii. Akili zao zimepotoka. Hawajui heshima ya kiutu ni nini. Tazama uhalifu … [Sehemu tupu katika kanda-Mh.] … ngono na kila kitu.

Na watazame wanawake wetu. Wamekuwa ghasia iliyoje. Tazama ni ghasia iliyoje ya ukosefu wa heshima na tabia za uasherati miongoni mwa wanawake zetu. Na sio tu hao …

Mnasema, “Hao ni Wamethodisti.” Hao ni Wapentekoste pia. Ni wote.

[102] Mtazame bibi Semple McPherson, Aimee Semple McPherson, aliyekuwa na hekalu hili. Kila mwanamke mhubiri alivaa hayo mabawa na kubeba Biblia jinsi huyu alivyofanya, uigaji wa kimwili tu!

Hawawezi kuwa halisi. Ndivyo makanisa yasivyoweza kuwa. Hebu kanisa moja hapa jijini lipate kitu fulani au kingine, kanisa hili lingine halitaweza kuvumilia. Nao watakipata. Mnaona? Wao si halisi tena.

Neno la Mungu ni halisi. Hilo ndilo Neno. Sharti lizae kwa namna yake, namna Yake katika majira Yake, teule, lililochaguliwa tangu asili na Baba Mungu.

[103] Sasa tunaingiaje katika kanisa hili? “Kwa Roho Mmoja sote tumebatizwa tuwe katika huu Mwili Mmoja, Mwili wa Kristo,” ambao ndio Bibi arusi, lile Neno. “Wamebatizwa mle kwa Roho Mtakatifu.”

[104] Sasa hebu tuangalie kama tuko katika kizazi cha mwisho au la. Sasa tunakuta, kama tukirudi nyuma katika Kitabu cha Mwanzo, kama ah, kama mlango wa 5, unaweza pia kufungua Luka na ukute kuwa Henoko alikuwa wa saba kutoka Nuhu. Henoko.

Hapo tunaudaka ule uzao wa nyoka. Kwani, kama Kaini alikuwa mwana wa Habili, basi yeye angelikuwa wa nane. Mnaona? Lakini hakuna mahali popote katika Biblia paliposema kuwa Kaini alikuwa mwana wa Habili … au Kaini-au Kaini alikuwa mwana wa Adamu. Kwa sababu, hiyo, Biblia ilisema, “Yeye alikuwa wa yule mwovu.” Na Adamu hakuwa yule mwovu. Mnaona? “Yeye alikuwa wa yule mwovu.”

[105] Sasa tunakuta hapa kuwa Henoko alikuwa wa saba kutoka Nuhu, hiyo ilikuwa mfano wa nyakati saba za kanisa. Sasa, wote waliosalia wa hao watu sita, waliokuwa kabla yake, walikufa, lakini Henoko alibadilishwa. Henoko alinyakuliwa, yeye akiwa wa saba, ikionyesha kuwa ni kipindi cha saba cha kanisa kitakachoingia kwenye Unyakuo. Sasa, hakuna shaka, tuko katika kipindi cha saba cha kanisa. Sote tunajua hilo.

[106] Sasa, ni kipindi cha Saba cha kanisa ndicho kinachoingia kwenye Unyakuo. Wale wengine sita wote walikufa. Lakini Henoko alibadilishwa, kwa sababu, “Alitoweka, Mungu alimtwaa.” Lakini Henoko aliyenyakuliwa, alikuwa mfano kwa wle wengine wote waliokufa. Lakini yule-Bibi arusi wa siku za mwisho ataitwa kutoka katika … Unyakuaji, bila kifo, wataitwa kutoka katika kipindi cha Saba cha kanisa, ambapo sisi tu washuhuda wa kizazi hicho sasa. Lo, jamani! Hebu tuchimbe ndani sasa, ndani kabisa. Mnaona?

[107] Sasa, hapa, pia, ni mfano wa vipindi saba vya kanisa , ambapo katika Ufunuo 10:7 kuwa lile fumbo kuu la kile Kitabu lingefunuliwa na Ujumbe wa malaika wa saba.

[108] Sasa, siku zote kuna Mjumbe wa juu na mjumbe wa duniani. Neno la Kiingereza *malaika* lamaanisha “mjumbe.” Na katika Ujumbe wa malaika wa saba, wakati alipokuwa anatangaza, huduma yake, “ndipo wakati alipoanza kupiga baragumu ya huduma yake,” siyo wakati alipoanza kuhubiri..

Yesu wakati alipoanza kuhubiri, Yeye alianza kuponya wagonjwa na waliokuwa matesoni. “Aah, yule Mwalimu Mkuu! Yeye ni Nabii” Kila mtu alimhitaji Yeye afike kanisani kwake.

Lakini Yeye alipoketi chini siku moja na kusema, “Mimi na Baba Yangu tu Mmoja,” hilo lilikuwa tofauti. “Na msipokula nyama ya Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, huna uzima ndani yako.”

“Mbona ni mnyonya damu!” Mnaona? Mnaona? Hilo lilikuwa tofauti.

Yeye hakulieleza hilo. Tayari walikwishaona udhihirisho, uthibitisho wa Neno la Mungu kwa kizazi Chake, likifanyika kuwa halisi na wao kuhakikishiwa kuwa Yeye alikuwa ndiye Mjumbe wa kipindi kile. Na haikumlazimu kueleza kitu chochote.

[109] Wale wanafunzi huenda hawakuweza kulieleza Hilo. Lakini waliliamini Hilo, kama waliweza kulielezea au la. Waliketi pale kwa utulivu na wakaliamini Hilo. Wangewezaje kusema walikuwa wanakwenda kula nyama Yake na kuinywa Damu Yake? Mbona, isingewezekana wao kufanya hivyo. Lakini waliamini Hilo, kwa sababu walikuwa wamepangiwa kimbele kuwa hivyo. Yesu alisema Ali “wachagua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Mnaona? Wao waliamini Hilo. Kama wangeliweza kulielezea au la, bado waliliamini Hilo.

[110] Sasa, tazama, sasa, katika kipindi cha saba, “Wakati malaika wa saba alipoanza kupiga baragumu, siri za Mungu zilipasa zifahamike pale pale” ile Mihuri.

Kwamba, wale watengenezaji wa kanisa walikuwa na wakati. Luther hakuishi kirefu vya kutosha, wala hata Wesley. Vile vipindi, yaani wale watengenezaji hawakuishi kirefu vya kutosha. Wao walikuwa na ujumbe wa siku yao, na watu walipokea na wakaufanya kuwa dhehebu. Na ni kitu gani?

[111] Huwezi ukaikandamiza asili. Asili siku zote hutoa ushuhuda. Mungu hupita katika mwendelezo wa asili. Sharti iwe hivyo.

Kama jua lilivyo. Jua linachomoza asubuhi, ni mtoto mdogo alyezaliwa. Ni dhaifu, halina joto jingi. Sasa nne linakuwa limehitimu shule ya juu. Wakati wa adhuhuri linaanza maisha. Saa tisa alasiri linaanza kuzeeka. Saa kumi na moja jioni liko kufani. Limekuwa zee na dhaifu tena, linarejea kaburini. Je, huo ni mwisho wake? Linafufuka tena asubuhi inayofuata. Mnaona?

[112] Hebu itazame miti, jinsi inavyochomoza majani yake, kila kitu inachokifanya. Sasa, tunakuta kuwa, majani hudondoka kutoka mtini, yanarejea. Nini? Uhai unakwenda chini hadi kwenye mizizi ya huo mti. Je huo ndio mwisho wake? Uhai unarejea tena kipindi cha theluji kikipita yakaja majira ya kuchipua na uhai mpya.

[113] Sasa, tazama makanisa, jinsi yalivyofanya kitu kile kile katika matengenezo. Imekuwa kuja juu. Ile chembe ya ngano ilianguka ardhini na ikafa katika mateso ya kipindi cha giza. Ilienda udongoni. Ilibidi ife. Mtu yeyote aliye wa kiroho ataliona hilo. Ile mbegu isipokufa na kuoza hukaa peke yake. Na ilibidi iingie kwenye udongo, chini ya kipindi cha giza. Ililala pale ikaoza. Na ilichomoza juu ikiwa vijani viwili vya Kanisa la Kilutheri. Kutoka Kanisa la Kilutheri vikachipua vijani vingi, Zwingli na kadhalika. Kutoka hapo ikakua ikawa shada, ambalo lilikuwa John Wesley, kipindi kikuu cha Umeshenari, likaangukia nyuma. Kutoka hapo kikaja kipindi cha udanganyifu, kile kipindi cha Upentekoste. Ile chembe ya ngano ile …

[114] Kuna mtu yeyote, hapa, aliyewahi kupanda ngano? Itazame ile ngano wakati unapoiangalia. Wakati unapotoka nje pale, unasema, “Nina ngano.” Unaona kama unayo ngano pale. Ufungue ganda lake kwa karibu kabisa na uone. Hunangano yoyote kabisa. Unalo kapi. Je, Yesu hakutuonya juu ya hilo katika Mathayo 24:22 … nne? “Katika siku za mwisho hizi roho mbili zitafanana sana, hata wateule wangedanganyika kama ingaliwezekana.” Mnaona? Sasa tazama. Huo ni mfuko wa kubebea.

[115] Sasa, Uhai uliokuja kupitia Luther ndio uliomfanya Wesley. Uhai uliotoka kwa Wesley ndio uliofanya Pentekoste. Uhai unaotoka Pentekoste ndio unaofanya ngano. Lakini hao ni wabebaji. Mnaona? Uhai wa kweli unapitia pale. Ujumbe unaendelea mbele, lakini unasonga mbele hadi kufanyika ngano. Hiyo ndiyo sababu ngano inapanda juu na kulileta jambo lote kwenye Unyakuo, juu hapa kileleni. Bibi arusi Mwenyewe anatoka katika kila kipindi. Lakini lile shina la kidhehebu linakufa, linakauka na kufa. Je, umegundua katika siku hizi za mwisho jinsi ambavyo ameanza kutoka humo sasa? Pindi ngano hiyo ianzapo kukua, ndipo-kapi linaanza kuachana nayo.

[116] Tazama nyuma katika ile ngano ndogo wakati unapoitazama. Pasua ganda hivi na uitazame na uone. Ndani kwenye mbegu unalo chipukizi la ngano. Ili kuliona unahitaji darubini yenye uwezo wa kuona mara thelathini zaidi ndipo ukaone hako kachipukizi nyuma pale. Unaona? Liko huko ndani mle, lakini linaanza kukua. Sasa, lile kapi sharti liwe pale ili kufunika ile, kuipa nafasi ipate kutoka nje. Lakini basi wakati inapoanza kukua na Ujumbe unaanza kuenea, ndipo kapi linajiondoa kutoka Kwake. Na uhai unaondoka moja kwa moja kutoka kwa lile kapi na kuingia moja kwa moja ndani ya ngano.